

# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA

**African Conference 2017 in Nairobi Kenya**



**Kutoka kwa Mhariri: Kongamano la Afrika Makabila 12 ya Waisraeli wako wapi?  
2017. Kanisa la Mungu Linaloendelea**

# Unabii wa Habari za Biblia

Aprili-Juni 2017

Katika makala hii

2. **Kutoka kwa Mhariri:** Kongamano la Afrika 2017. Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) lilikuwa na kongamano la baadhi ya viongozi wake mwaka huu wa 2017.

3. **Makabila 12 ya Waisraeli wako wapi?** Wakati wengi wanajua wanakopatikana kabila la Yuda, wengi hawajui mahali makabila 12 wako (pamoja na "makabila nusu") ama walikoenda.

16. **Vidokezi Ishirini na Vinane vya Maombi Yanayofaa:** Sehemu ya 7. Je, ungependa kujifundisha jinsi ya kufanya maombi yako yafae zaidi?

22. **Somo la 12. Kozi ya Biblia: Thibitisho la Historia ya Biblia-Utambulizi.**

27. **Pasaka:** Je, Inahusu Kifo cha Yesu pekee? Je, Wakristo wanapaswa kuadhimisha Pasaka?

**Jalada la Nyuma: Intaneti na Redio:** Hii inaonyesha watu mahali pa kupata ujumbe wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG).

Kuhusu Jalada la Mbele:  
Picha hizi zilitoka kwa  
Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG)  
Jijini Nairobi, Kenya.

Unabii wa Habari za  
Biblia inachapishwa na  
Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG),  
1036 W. Grande Avenue,  
Grover Beach, CA,  
93433. [https://  
www.ccog.org](https://www.ccog.org).

©2017 Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG).  
Imechapishwa  
Marekani. Haki zote  
zimehifadhiwa.

Kunakili makala yote  
ama sehemu yake pasipo  
ruhusa ya kimaandishi  
toka kwa mmiliki  
hairuhusiwi.

Tunaheshimu haki zako  
hivyo hatutoi, kuuza  
ama kukodisha orodha  
ya mawasiliano yetu.  
Endapo haungependa  
kuupokea gazeti hili,  
wasiliana na afisi yetu  
ya Grover  
Beach. Maandiko  
yamenukuriwa toka New  
King James Version  
©Thomas Nelson, Inc,  
Publishers, inatumika  
kwa idhini isipokuwa  
pale tu tumelekezwa  
vinginevyo.

Unabii wa Habari za  
Biblia HUWEZESHA KWA  
MICHANGO YENU

**Mhariri Mkuu: Bob Thiel**

**Makala/Mhariri  
Mzaidizi: Joyce Thiel**

**Mashahihisho: John  
Hickey; SBC Msaidizi wa  
kozi; Shirley Gestro.**

**Picha: Picha zote  
zimetokana na familia  
ya Thiel ama na vyanzo  
vya mitandao ya kijamii  
kama vile Wikipedia  
ama serikali fulani  
(isipokuwa sifa  
imetolewa).**



**KUTOKA KWA MHARIRI  
MKUU: BOB THIEL**

**Kongamano la Afrika  
2017.**

Katika Februari 2017, Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) lilifanya kongamano la baadhi ya viongozi wetu Afrika jijini Nairobi, Kenya.

Kwa sababu ya upungufu wa bajeti yetu, hatungeweza kukutana na viongozi wote. Lakini tuliweza angalau kukutana na mwakilishi mmoja kutoka Ghana, Malawi, Msumbiji, Tanzania na viongozi wengi kutoka Kenya.

Tulikuwa tunataka viongozi kutoka maeneo tofauti wapate kukutana pamoja, na pia kukutana na mimi na Aleksandar Veljic aliyetoka Serbia. Kabla ya kongamano, Aleksandar Veljic, alichukua muda wa wiki moja na Mchungaji Mwangalizi Evans Ochieng akiwatembelea waumini wa maeneo mbalimbali nchini Kenya. Aliweza kuona umaskini, matumaini na ukuaji wa kiroho katika maeneo mengi.

Tuliongoza mihadhara katika mada tofauti, kama vile kwa nini Kanisa la kweli la Mungu linahusu upendo, ukweli, ufalme wa Mungu, historia, unabii, na kufikia watu katika lugha tofauti. Kulikuwako na kuwekewa wakfu wa aina nyingi na "kuwekewa mikono" (Timotheo 1:6).

Pia nilitoa mafunzo kuhusu mafundisho na kupitia tofauti ulioko kati ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) na vikundi vingine vya Sabato kama vile Wadvestista wa Kisabato (SDA), Wadvestista wa Batiso, Kanisa la Mungu (La Sabato) - CoG7, na vikundi vingine ambavyo

viongozi wao walikuwa sehemu ya Kanisa la Mungu Ulimwenguni Kote (WCG). Tulieleza pia kuhusu tofauti kati yetu na Waprotestani wengine, Othodoksi wa Mashariki na Wakatoliki wa Rumi na kuyajibu maswali mengine.

Hapo awali mnamo 2014, tuliweza pia kuandaa kongamano jijini Nairobi. Wakati huo tulikuwa na viongozi kutoka Kenya na mmoja kutoka Tanzania aliyehudhuria. Tulikuwa na waumini wapatao 260 wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) katika nchi hizo mbili.

Tangia wakati huo, waumini wetu wameongezeka hadi karibia 2000. Wakati Mungu anaita (Yohana 6:44; 1 Wathesalonike 2:12), hii kwa kawaida imefanyika kupitia kwa watu wanaosoma makala yangu na pia Mchungaji Evans Ochieng anayetembelea maeneo mengi na kuwaambia ujumbe ambao sisi tulio katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) tunafanya na kuamini kupitia kwa misaada ya wengine.

Sambamba na yaliaoandikwa na Mtume Paulo, napanda, Mchungaji Ochieng anaita maji bali mwenye kukuza ni Mungu (1 Wakorintho 3:6).

Kwa sababu ya bidii yake ya uinjilisti, Mchungaji Evans Ochieng aliwekwa wakfu kama Muinjilisti kwa mwelekeo wangu wakati huo wa kongamano. Huku ndiko kuwekewa wakfu wa kipekee katika Kanisa letu. Tunaendelea kufikia watu wengi katika Afrika na tunatarajia kuona ukuaji mwingi katika siku zijazo.

## Makabila ya Israeli Kumi na wawili Wako Wapi?



*Bango la Musa la Makabila 12 ya Waisraeli. Kutoka Gifati Mordekai Et2 mbele ya sinagogi la Yusufu, barabara ya dhahabu ya Ha Rav, katika Yerusalemu. Mstari wa juu, kulia hadi kushoto: Asheri, Dani, Reubeni; katikati: Yosefu, Naftali, Isakari, Simeoni; Chini: Benyamini, Gadi, Zabuloni, Lawi.*

Na Bob Thiel

Biblia inarekodi kwamba Yakobo, ambaye pia aliitwa Israeli, alitabiri kuhusu "makabila nusu" 2 ya Efraimu na Manase katika Mwanzo 48, ambao walikuwa wana wa mtoto wake Yosefu. Biblia pia inaonyesha kwamba alitabiri kitakachowapata makabila kumi na wawili ambao walitoka kwa vijana wake kumi na wawili.

Wakati watu wengi wanakubali utambulisho wa kabila moja (Yuda), wachache wanaonekana hawaelewi utambulisho wa makabila mengine ama kwa nini habari hii inawezakuwa ya muhimu.

Hizi ni rekodi za Biblia katika Mwanzo 49 za unabii wa SIKU ZA MWISHO wa ukoo wa Yakobo:

1 Yakobo akawaita wanawe, akasema, Kusanyikeni, ili niwaambie yatakayowapata siku za mwisho.

2 "Kusanyikeni, msikie, enyi wana wa Yakobo, Msikilizeni Israeli, baba yenu.

3. "Reubeni, u mzaliwa wangu wa kwanza, nguvu zangu, na malimbuko ya uwezo wangu. Umewapitia wengine kwa ukuu na kwa nguvu. 4 Umeruka mpaka kama maji, basi usiwe na ukuu, kwa sababu ulikipanda kitanda cha baba yako, ukakitia unajisi; alikipandia kitanda changu.

5 Simeoni na Lawi ni ndugu; panga zao ni silaha za jeuri. 6 Nafsi yangu, usiingie katika siri yao, Fahari yangu usiungane na kusanyiko lao. Maana katika ghadhabu yao walimuua mtu, Na kwa ukaidi wao walikata mshipa wa ng'ombe; 7 Ghadhabu yao na ilaaniwe, maana ilikuwa kali haina huruma. Nitawagawa katika Yakobo, Nitawatawanya katika Israeli.

8 Yuda ndugu zako watakusifu, Mkono wako utakuwa shingoni mwa adui zako. Wana wa baba yako watakuinamia. 9 Yuda ni mwana-simba, kutoka katika mawindo, mwanangu umepanda; Aliinama akajilaza kama simba, Na kama simba mke; ni nani atakaye mwamsha? 10 Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, Wala mfyanyasheria kati ya miguu yake, Hata atakapokuja Yeye, mwenye milki, Ambaye mataifa watamtii. 11 Atafunga punda wake katika mzabibu, Na mwana-punda wake katika mzabibu mzuri. Amefua nguo zake kwa mvinyo, Na mavazi yake kwa damu ya zabibu. 12 Macho yake yatakuwa mekundu kwa mvinyo, Na meno yake yatakuwa meupe kwa maziwa.

13 "Zabuloni atakaa pwani ya bahari, Naye atakuwa kama pwani za kuegesha merikebu, Na mpaka wake utakuwa kando ya Sidoni.

14 "Isakari ni punda hodari, Ajilazaye kati ya mazizi ya kondoo;15 Akaona mahali pa raha, kuwa pema, Na nchi, ya kuwa ni nzuri, akainama bega lake lichukue mizigo, akawa mtumishi kwa kazi ngumu.

16 "Dani atahukumu watu wake, kama moja ya makabila ya Israeli;17 Dani atakuwa nyoka barabarani, Bafe katika njia, Aumaye visigino vya farasi, Hata apandaye ataanguka chali.

18 "Wokovu wako nimeungoja, Ee BWANA.

19 "Gadi, jeshi litamsonga, Lakini atawasonga wao mpaka visigino.

20 "Asheri, chakula chake kitakuwa kinono, Naye atatoa tunu za ufalme.

21 "Naftali ni ayala aliyefunguliwa; anatoa maneno mazuri,

22 "Yusufu ni mti mchanga wenye kuzaa,Mti mchanga wenye kuzaa karibu na chemchemi,Matwi yake yametanda ukutani.23 Wapiga mishale walimtenda machungu,Wakamtupia,wakamwudhi,24 Lakini upinde wake ukakaa imara,Mikono yake ikapata nguvu,kwa mikono ya Mwenye Enzi wa Yakobo,kwa jina la Mchungaji.yeye jiwe la Israeli,25 Naam,kwa Mungu wa baba yako atakaye kusaidia;kwa mibaraka ya maziwa,na ya mimba.26 Mibaraka ya baba yako,imepita mibaraka ya milima ya kale,vitu vinavyotamanika vya vilima vya milele;Na vikae juu ya kichwa cha Yusufu,Juu ya utosi wa kichwa chake aliye mkuu kati ya ndugu zake.

27 Benyamini ni mbwa-mwitu mwenye kuraru-rarua. Asubuhi atakula mawindo, Na jioni atawagawanya mateka.

28 hizo zote ndizo kabila za Israeli kumi na mbili. Na hayo ndiyo aliyowaambia baba yao, na kuwaabariki; mmoja mmoja kwa mbaraka wake aliwabariki. (Mwanzo 49:1-28)

Tazama pia ifuatayo iliyoandikwa na nabii Isaya:

8 Nawe, Israeli, mtumishi wangu; Yakobo niliyekuchagua; mzao wa Ibrahimu, rafiki yangu;9 wewe niliyekushika toka miisho ya dunia, na kukuita toka pembe zake, nikikuambia, Wewe u mtumishi wangu; nimekuchagua wala sikukutupa, 10 usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu. (Isaya 41:8-10)

6 naam. asema hivi, Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejesha watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia. (Isaya 49:6)

Kumbuka kwamba kila kabila lilikuwa na "baraka" zake na wazao wengine wangekuwa katika miisho ya dunia. Kwa hivyo, kibiblia, wanafaa waangaliwe kila mmoja wao kibinafsi. Je, Uingereza, Kanada, Australia, nikitoe mifano mitatu, ziko miongoni mwa miisho ya dunia kutoka palestina 7 Na bado ukizingatia mashamba kama vile Fakilandi, na awali kama Mashariki ya mbali na Hindi, ambazo zilitawaliwa na Uingereza, baadhi ya makabila walitawanyika kwenye miisho ya dunia na mtawanyiko ujao utakaofanyika.

Yairi Davidi aliandika kwamba rabi aliyelitwa Manase ben Israeli katika karne ya 17 alipata kwamba neno la Ufuransa ya Uingereza, Angleterre, linamaanisha "Mwisho wa Dunia" (Davidy, UK.p.414)

Kama vile unabii wa Mwanzo unavyoenda, inasemekana:

Mataifa yaliyotambulika...kama mbegu ya Waisraeli wa Ibrahimu na haswa wale walioongoza sera za kikoloni kutoka karne ya kumi na nane hadi karne ya ishirini. (Davidy.The Tribes, p.15)

Ijapokuwa sikubaliani na maoni yote yaliyoandikwa kwenye kitabu kilichoandikwa hapo juu, imeandikwa:

Katika Sasia (Sinthia Mashariki) WARABANI wa Reubeni wamepakana na Giriani wa Gadi...Ribuiari-pia ni aina ya Reubeni...Ribuari walikuwa sawa na Wafaransa waliochukua jina lao. (Davidy.The Tribes, pp.161-162).

“WACHATI SITHAI”...Rekodi ya China inasema kwamba sehemu ya Wanaftali ambao waliishi Kaskazini mwao walighura kuelekea Magharibi kabla ya mwaka 450.Pia wanasema kwamba hapo awali walikuwa Kaskazini mwa Mlima wa Altai na walikuwa sehemu ya Masageti, waliokuwa na macho ya buluu na nywele nyororo (Davidy.the Tribes, pp.199-200).

Ufini limetambulika...kama...hasa Isakari (Davidy, The Tribes, p.217)

BENYAMINI pia linaonekana limeonyeshwa kuwa ni WANOMANI (Davidy.the Tribes, p. 232).

Uingereza ilitawaliwa na kabila la Yusufu na hasa sehemu ya Efraimu-walowezi wengi wanaoishi Afrika Kusini, Nyuzilandi, Australia na Kanada (Davidy.the Tribes, P. 403).

Wayalandi wa leo wana tabia kama za Dani na Simeoni...Babu za Danesi katika mila ya Wadani alitwa DANI (Davidy.The Tribes, p 432,438).

HALI YA WAISRAELI NA WAYAHUDI...Wayahudi wengi walitoka kwa kabila la Yuda wakifuatwa na kabila ya Benyamini na Simeoni pamoja na Walawi...Yuda ndiye kipengele cha kubainisha (Davidy.The Tribes, p.433).

Wafaransa hasa walitoka kwa Reubeni (Davidy.The tribes, p.440).

Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) twaamini kwamba ukoo wa Waisraeli walisafiri sehemu nyingi. Wakati orodha ifuatayo inahitaji marekebisho,

kimsingi inaonyesha mahali wengi wetu tumefundishwa kuhusu maeneo ukoo wa Israeli walienda. (Hata hivyo baadhi yao wametawanyika kote katika maeneo mengi):

Reubeni-Ufaransa (Wameheshimika, lakini wana matatizo, Mwanzo 49:3-4).

Yuda-Taifa linaloitwa Israeli leo hii na Wayahudi ambao hawapo katika eneo hilo lakini walitoka karibu na Yerusalemu (Ezra 4:12).

Simeoni-Wametawanyika kote katika makabila haya (Mwanzo 49:5).

Lawi-Wametawanyika kote katika makabila haya (Mwanzo 49:5).

Isakari-Ufini (ipatikanayo kati ya Uropa na Urusi, Mwanzo 49:14).

Zabuloni-Uholanzi (Pwani ya bahari, Mwanzo 49:13) na wachache walioko Afrika Kusini.

Gadi-Uswisi (wataendelea kwa muda mfupi kukubali utawala wa Uropa, Mwanzo 49:19).

Dani-Denmaki, (nje kidogo, Mwanzo 49:17 kabila lililompa jina mahali pao Dani; Waamuzi 18:12,29) (Wale wanaoishi Irelandi hasa ni ukoo wa Efraimu).

Asheri-Ubelgiji, Lusembagi (Mwanzo 49:20).

Napftali-Uswidi (ameelezwa kwa njia ya kuvutia, Mwanzo 49:21).

Benyamini-Norwe, isilandi (Wavikingi wa zamani, Mwanzo 49:270).

Efraimu- Uingereza,Kanada,Australia,Nyuzilandi na wengine walioko Afrika Kusini na Zimbabwe (Kundi la mataifa,Mwanzo 48:19).

Manase-Marekani (Taifa lililobarikiwa, Mwanzo 48:19).



Hizi ndizo nchi ambazo zina miji ya Israeli ambayo Yesu alitaja katika Mathayo 10:22-23.

Nchi kama Uswidi, Ubelgiji, Lusembagi, Norwe, Uswizi, Ufini, Ufaransa, Denmaki, Irelandi, Isilandi zinaonekana zafaa baadhi ya maelezo chanya katika Mwanzo 49-lakini baadaye zitapitia mitihani na majaribio kutoka kwa utawala wa Mnyama wa Uropa unaokuja (Ezekieli 5:4;39:23,28).

Pengine inafaa ionyeshwe kwamba "mataifa ya Waisraeli" wengi kikabila ni mchanganyiko (kulingana na Davidy. the Tribes, 4<sup>th</sup> edition. Rusell-Davidy Publishers, 2011 and other sources) na itawachukuwa muda ili Waisraeli halisi watengane.

Huenda pia wapatikane mahali ambapo watu 144,000 kutoka Ufunuo 7 watachaguliwa (isipokuwa Dani, ambaye hayuko katika orodha ya Ufunuo 7:4-8; kinachoshangaza ni kwamba wengi katika Kanisa la Katoliki wanaamini kwamba mpinga Kristo wa mwisho atatoka kwa kabila la Dani).

Awali katika Kanisa la Mungu Ulimwenguni Kote (WCG), wengine walikisia kwamba Denmaki wangejiondoa kwenye Umoja wa Ulaya na kutokuwa sehemu ya utawala wa Mnyama wa Uropa. Sina uhakika kwa njia yo yote wakati huu, lakini nadhani kwamba kuna uwezekano (maoni kuhusu nyoka na bafe katika Mwanzo 49:17 yamependekeza kwamba Dani ni tofauti kuliko wengine ambao wanaweza kuungana). Bado ukweli ni kwamba kabila la Dani ndilo kabila pekee ambalo halijatajwa miongoni mwa watu 144,000 katika Ufunuo 7:4-8, hiyo inafanya niegemee upande mwingine kwa sasa hivi-bado ukweli kwamba Denmaki hawajaanza kutumia Euro (Sarufu yao inahusiana nayo) inaonyesha yakini uhuru ulioko nje kidogo ya Umoja wa Uropa-lakini mpangilio huu hautadumu.

Kwa upande mwingine, sisi tulio masalio ya Filadelfia, na Kanisa la awali la WCG, tuligundua sahihi kwamba hawatadumu katika Umoja wa Ulaya na wangejiondoa.

Unabii wa Biblia unaonyesha wazi kwamba Uingereza halitakuwa mmoja wa MATAIFA yanayounda Muungano wa Mataifa ya Ulaya (McNair R.A Strong United Europe. Tomorrow's World, February 1970, p.17).

Inafaa ieleweke kwamba hatimaye Uingereza HAITASTAWI kama sehemu ya Umoja wa Ulaya lakini watabadilishwa na mamlaka ya mnyama wa Uropa wa mwisho-na bado aliyekuwa Waziri Mkuu anaendeleza kitu ambacho hakitasaidia Waingereza. (Thiel B. Tony Blair calls for a Strong Elected EU President. Church of God News, June 9, 2007.)

Pengine inafaa itajwe kwamba msimamo kwa ujumla ulioko katika makanisa ya Mungu ni kwamba Uingereza hawatabaki katika Umoja wa Uropa na watajiondoa baadaye. (Thiel B. Tony Blair a Catholic EU Leader? Church of God News, June 26, 2007).

Hapo awali mnamo 1990, nikiwa makamu wa Rais wa Utengenezaji wa vifaa vya kunyunyizia maji, nilimwambia mwakilishi wa mauzo yetu aliyekuwa Mwingereza, aliyetembelea Kiwanda chetu cha Kalifonia, kwamba siku moja Uingereza watajiondoa kwa Uropa. Alikataa na kuniambia kwamba jambo hilo haliwezekani. Na alitoa sababu lakini si za kibiblia-nikamwambia kwamba alikuwa kwa upotofu. Kura uliopigwa na Uingereza kujiondoa kwa Umoja wa Uropa mnamo Juni 23, 2017 (inayoitwa Brexit), inaonyesha kwamba huyu mwakilishi wa mauzo, ambaye hakuwa katika Kanisa la Mungu, alikuwa upotofuni.

## **Muundo wa Israeli katika Mwaka wa 1948**

Inafaa ionyeshwe kwamba wengi kawaida wanaamini kuwa taifa la Wayahudi linaloitwa Israeli ndio WAISRAELI WOTE, pamoja na Wayahudi waliotawanyika ulimwenguni kote. Vile yanavyoonyeshwa na maandiko mengine (K. v Mwanzo 48:11,15-16,19-20;1 Mambo ya Nyakati 5:1-2), jina Israeli lilipewa ukoo wa Yusufu.Na bado lilitabiriwa kwamba watawaita Wayahudi “Israeli”

1 Sikieni haya, enyi watu wa nyumba ya Yakobo, mnaoitwa kwa jina Israeli, mliotoka katika maji ya Yuda (Isaya 48:1).

Tendo hili limefanyika leo, kwa hivyo wengi wamepuuzia maandiko yanayofundisha kwamba kuna makabila mengine ya Israeli katika maeneo mengine (Yakobo 1:1).

Wakati wengine wametaja muundo wa taifa dogo la Israeli kama utimizaji wa unabii mwingi wa siku za mwisho, kauli hii mara kwa mara imezungumzwa zaidi.

Ijapokuwa muundo huu una umuhimu, haukuwa “mti” ambao Waprotestani wengi wanaochambua unabii wamedai kwamba ni mwanzo wa kizazi cha mwisho (Marko 13:28-30). Tukijua kwamba kizazi kinaweza kuchukua miaka 70 (Zaburi 90:10), Yesu angehitaji kurudi mwaka 2018 kama 1948 ndio mwaka wa kuanzia “kizazi hiki hakitapita, hata haya yote yatimie” (Mathayo 24:34; Mariko 13:30).

Zaidi ya hayo, muundo wa Israeli sio kusanywa tena ambako Waprotestani wengine wanadai. Herbert Armstrong aliandika yafuatayo katika mwaka wa 1948;

### **Sio Ukusanyaji Uliotabiriwa Kufanyika Tena**

Kwa wakati unaofaa wa Mungu,Wayahudi wataachiliwa kutoka kwa mateso

yao,majaribu ya kuogofya na kuwekwa imara tena katika Palestina kwa IMANI! Lakini huu sio ukusanyaji tena wa Israeli.Hii tu ni bidii ya kijinga ya wanadamu ya kufanya hivyo kabla ya wakati, badala ya kumgonja Mungu kuwafanyia. Na harakati hii ya sasa ya kuunda taifa la Wayahudi na kuliita “ISRAELI” inaweza kuzua umwagikaji wa damu na matatizo mengi.

Hata hivyo, taifa jipya lililojitangaza kama Palestina silo Israeli hata kidogo-ni sehemu tu ya YUDA! Wakati uhamisho mkuu utafanyika, litakuwa taifa ya Israeli na Yuda pamoja. Na hawatafanya hivyo kupitia uasi wao, mamlaka yao ya chuki na nguvu zao, watarudishwa na Kristo baada ya kurudi kwake, kutoka kwa hali ya utumwa na kutoka kwa nchi za maadui zao (tazama Ezek.39:25-27. Wakati huo watawateka watekaji wao na kuwatawala wale waliowatawala (Isaya 14:1-3-tazama hasa tafsiri ya Mofati; Yeremia 30:16; 31:11). Utakuwa uhamisho mkubwa kuliko ule uliofanywa chini ya Musa-huu utakuwa chini ya mamlaka ya KRISTO atakaporudi! (Yeremia 23:7-8).

Watarudi Palestina wakiomboleza, wakuingama dhambi zao, wakijichukia vile walivyopuuzia na kutenda maovu dhidi ya Mungu, wakitafuta MASIHI waliomkana (Yer.50:4-5; Ezek.20:34-43). Baadaye watabadilishwa kugeuka kutoka dhambini hadi watu waliojaa na Roho na kuishi kwa amri za Mungu (Yer.50:19-20, Ezek.36:24-28). Wayahudi walioko Palestina na taifa jipya halitimizi unabii WO WOTE HUO! Ni mashaka gani haya ya ajabu!

### **Wayahudi sio Waisraeli**

Watu wengi wanaonekana hawajui kwamba wayahudi sio Waisraeli,lakini ni sehemu tu ya Yuda.Sehemu ya kwanza ambayo neno “Wayahudi” lilipatikana ni wakati Wayahudi walikuwa na vita dhidi ya WAISRAELI ( 2 Wafalme



16:6). Vitabu vinne mzima katika Biblia vimeonyesha tofauti kati ya mataifa ya Israeli na Yuda. Kulikuwako na makabila kumi na mawili, hapo awali. Lakini baada ya kifo cha Sulemani, taifa la ISRAELI walikataa mfalme wao, Rehoboamu, mwana wa Sulemani, na kumfanya Yeroboamu, kabila la Efraimu, mfalme. Halafu kabila moja la Yuda likatoka kwa taifa la Israeli na kuliunda TAIFA JIPYA lao (vile wanavyojaribu kufanya leo), ili wazidi kudumisha Rehoboamu kama mfalme. Taifa hili jipya liliitwa ufalme wa YUDA. Kabila la Benyamini na sehemu kubwa ya Lawi likaungana na Yuda, na MAKABILA kumi yakaunda taifa linaloitwa ISRAELI. (Armstrong HW. Plain Truth, June 1948).

Na alisema ukweli. Taifa la Israeli halionyeshi makabila yote ya Waisraeli. Tazama pia unabii unaofuata:

18 "Siku zile nyumba ya Yuda watakwenda pamoja na nyumba ya Israeli, nao watakuja pamoja, kutoka nchi ya Kaskazini, mpaka nchi ile niliyowapa baba zenu iwe urithi wao. (Yeremia 3:18)

7 Maana BWANA asema hivi, Mwimbieni Yakobo kwa furaha, mkampigie kelele mkuu wa mataifa, tangazeni, sifuni, mkaseme, Ee BWANA, uwaokoe watu wako, mabaki ya Israeli. 8 Tazama, nitawaleta toka nchi ya Kaskazini, na kuwakusanya katika miisho ya dunia, na pamoja nao watakuja walio vipofu, na hao wachechemeao, mwanamke mwenye mimba, na yeye pia aliye na utungu wa kuzaa; watarudi huko, jeshi kubwa. 9 Watakuja kwa kulia, na kwa maombi nitawaongoza; nitawaendesha

penye mito ya maji, katika njia ilionyooka; katika njia hiyo hawatajikwaa; maana mimi ni baba wa Israeli, na Efraimu ni mzaliwa wa kwanza wangu. 10 Lisikieni neno la BWANA, enyi mataifa, litangazeni visiwani mbali; mkaseme, Aliyemtawanya Israeli atamkusanya, na kumlinda kama mchungaji, alindavyo kundi lake (Yeremia 31:7-10).

Huo HAUJATIMILIKA. "Nchi ya Kaskazini" ni Babeli ya nyakati za mwisho inayoitwa Uropa (Zekaria 2:6-7).

Kwa sababu wengine hawaelewi kwamba taifa linaloitwa Israeli silo Waisraeli wote, wamekosa kufahamu wakati unabii kama ya Ezekieli 38 utatimilika.

#### **Maoni Mengine Kuhusu Makabila**

Wengine wanakataa dhana mzima ya makabila kuwa ni wazungu na wanasema kwamba watu tofauti/makabila/mataifa mara nyingi wanaonekana tofauti kuliko Wayahudi. Lakini kumbuka yafuatayo:

11 Basi kama ukamilifu ulikuwapo kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo); kulikuwa na haja gani tena kuhani mwingine ainuke, kwa mfano wa Melkizedeki, wala asihesabiwe kwa mfano wa Haruni? 12 Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike. 13 Maana yeye aliyenenwa hayo alikuwa mshirika wa kabila nyingine, ambayo hapana mtu wa kabila hiyo aliyeihudumia madhabahu. 14 Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakunena neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani (Waebrania 7:11-14).

Kwa vile ni dhahiri kwamba Yesu alifanana na Myahudi (kutoka Yuda) na siye Mlawi (kabila ambayo makuhani

walitokea) Agano Jipya linaonyesha dhahiri kwamba waliotoka Yuda wangetofautishwa na kabila la Lawi.

Kwa hivyo ni wazi kwamba watu wa kabila mbalimbali ya Israeli, hata sasa, wanatofautiana. Kwa sababu ya kuoana na mambo mengine, nchi zingine ambazo kabila tofauti zimemiliki zinaleta mada ya mjadala-hata hivyo, kwa ujumla watu wa Ulaya wanaonekana walitoka kwa kabila za Israeli kama vile mataifa yaliyotoka kwa hao.

Haya ni maoni mengine kutoka kwa hayati Dk. Hoe kuhusu utambulisho wa makabila mengine (niliacha Efraimu, Manase, na Yuda kwa vile hawana habari mahali pengine):

4 Walawi, kabila la makuhani, wangetawanyika katika Israeli (Mwanzo 49:5-7). Mungu hakuwapa nchi la kulirithi kama vile makabila mengine. Kwa hivyo tusitarajie wamepeva eneo la kurilirithi leo hii. Hakuna yaliyosemwa katika Kumbu Kumbu 33 kuhusu umilikaji wao wa nchi miongoni mwa Wayahudi leo hii, tunapata wengi wanaoitwa Lawi, Levi na Levina, wengine jina "koheni" na mengine tofauti. Neno la Kiebrania "koheni" linamaanisha kuhani na limetafsiriwa mara 725 katika KJV. Hapa basi tuna Walawi wengi waliotawanyika miongoni mwa Yuda kwa sababu waliacha kazi yao ya ukuhani kabisa katika Israeli (1 Wafalme 12:31).

5 Simeoni hakupata Baraka yo yote kutoka kwa Musa. Kwa hakika, hajataja kabila hiyo! Yakobo alisema Mungu atawatawanya kote katika Israeli. Kwa jinsi gani? Ukichukua ramani ya Palestina ya wakati wa mgawanyiko wa nchi, utapata kwamba Simeoni hakuwa na urithi KUSINI mwa Yuda. wakati Yuda alitengana na Israeli, Yuda alichukua wilaya iliyoteuliwa wa Simeoni. Kabila hili likatawinyika. Kuna uwezekano kwamba kabila dogo lililoko Magharibi ya Uropa, ambalo mara nyingi wanaitwa

Senonisi au Semonisi, wanawakilisha sehemu za kabila la Simeoni.

6 Reubeni, usiyezuiwa kama maji asiwe mkuu tena, tumegundua ni Ufaransa. Ufaransa wa Kusini, Kunakoishi ukoo wa Javani (Wagiriki), ni wamataifa-wanayumba kama maji, na bado wana mitindo ya ulimwengu, wana aina ya ufasaha kamili, na wana udhaifu wa kimapenzi kama Reubeni, ni Ufaransa... na siyo muhimu kwamba nchi ambayo ilikuwa na vita na Uingereza mwaka wa 1800 ilikuwa ni Ufaransa (Reubeni) ambayo ilipoteza haki za kuzaliwa katika vita vya Napoleoni (Napoleoni alikuwa Mtaliano).

7. Dani awali iligawanyika mara mbili, moja karibu na Jopa, bandarini, na nyingine kwenye Kaskazini mwa Palestina. Dani walikataa kupigana na makabila mengine dhidi ya mataifa (Waamuzi 5:17). Dani angehukumu ama kusimama kutawala watu wake kama kabila tofauti ya Israeli kuonyesha kwamba angejipatia serikali yake mwenyewe kwa njia ifuatayo: "Dani atakuwa nyoka barabarani, Bafe katika njia aumaye visigino vya farasi-Hata apandaye ataanguka chali." Irelandi wamefanya hivyo kwa Waingereza. Hakika ishara isiyo halali ya jeshi la Jamhuri ya Kiarishi ni nyoka aliyejikunja.

Dani pia angekuwa kama shibli arukaye, maelezo ya Denmaki ambao walinunua visiwa bikira, Grinilandi, Isilandi wakati wao wa neema. Cha kipekee hasa ni ukweli kwa makabila yote, Dani wa Kaskazini bado wanahifadhi jina la baba yao Danesi!

Benyamini inaunda Norwei na Isilandi. Watu wa Isilandi kwa hakika ni koloni ya Wanorwe. Benyamini alipewa Daudi kwa sababu Yerusalemu, Jiji kuu la Daudi, lilikuwa katika kabila la Benyamini, sio Yuda. Mungu alisema atampa Daudi taa katika Yerusalemu (1 Wafalme 11:36). Mstari huu haukuashiria

Yuda ambayo haikupewa nyumba ya Wayahudi. Benyamini aliambiwa akimbie kutoka kwa uharibifu wa Yerusalemu (Yer. 6:1) ambao wengi walifanya.

Benyamini amefananishwa na “mbwa-mwitu mwenye kurarua-rarua Asubuhi atakula mawindo, na jioni atagawanya mateka” (Mwanzo 49:27). Haya ni maelezo sahihi ya Wavikingi ambao waliteka nyara Uropa wa Kaskazini, na hata maeneo ya Mediterania. Mashambulizi karibu yote yalitoka Norwei. Ni ya muhimu kwamba Benyamini, ambao ni kabila dogo, bado ni dogo hadi leo. Kuna Wanorwei wachache (pamoja na elfu 148 kutoka Isilandi) kuliko taifa lo lote Israeli. (Baraka za Musa katika Kumbukumbu 33 zina kumbukumbu maalumu kwa ukweli huu kwamba jiji la Yerusalemu lilikuwa katika kabila la Benyamini.)

9. Isakari amelinganishwa na “punda hodari,” Yakobo anaendelea: “akaona mahali pa raha, kuwa pema, Na nchi, ya kuwa ni nzuri AKAINAMA BEGA LAKE LICHUKUE MIZIGO, akawa MTUMISHI KWA KAZI NGUMU.” (Mwanzo 49:14-15). Punda siye mnyama mwerevu sana kwa wanyama, lakini anapenda kufanya kazi. Hii ni nchi ya Ufini. Ufini ndilo taifa PEKEE ambalo limefanya bidii ya kulipa deni yake. Nchi hii inalipa fidia kubwa kwa Urusi. Shamba lake ni jema na la kupendeza, lakini silo tajiri sana. Kulingana na Kumbukumbu 33:19 anautoa utajiri kutoka kwa uvuvi na hazina zilizofichwa za mchanga mkubwa na mchanga mnyororo wa kuutengeneza vioo. Isakari sio walowezi, wanaishi kama wachungaji “hemani,” vile Musa alivyosema.

10. Naftali amefananishwa na Uswidi “ametosheka na fadhila, yuna Baraka kutoka kwa Bwana.” Amefananishwa na ayala aliyefunguliwa, “anatoa maneno mazuri.” (Mwanzo 49:21). Kwa Uswidi, na uchumi mzuri, linatoka tuzo la Nobeli kwa ishara ya ufanikishaji mkuu wa

ulimwengu. Uswidi, wakati wa vita vya ulimwengu na taabu zilizotokea hivi karibuni kule Palestina, iliwatumia wajumbe kuongea maneno ya upatanisho na amani. Ahadi ya Musa kumiliki “bahari na kusini” inafaa kwa Naftali wa zamani na Uswidi wa leo: tazama mahali Bahari ya Galilaya na Baltiki ukilinganisha na mahali pa kabila hili.

11. Zabuloni waliishi Uholanzi (Netherlands). Zabuloni anakaa “pwani ya bahari, naye atakuwa kama pwani za kuesha merikebu, na mpaka wake utakuwa kando ya Sidoni” Nchi ya mataifa. Musa alisema: “Furahini, Zabuloni, kwa kuenda kwako nje.” Anachukua pia hazina kutoka kwa bahari na mchanga, Zabuloni, basi ni walowezi. Sio watekaji nyara kama Benyamini.

12. Gadi, ambalo linamaanisha “kikosi” kwa hakika inaonyesha Uswisi taifa pekee la Israeli ambalo kila mtu anajihamasisha kiulinzi. Dhidi ya Gadi vitakuja vikosi vya kigeni, asema Yakobo lakini “atawasonga wao mpaka visigino.” Musa alisema kwamba Mungu HAWEZI “kuruka” tabia ya makabila walowezi ama wanaoteka nyara. Gadi “hurarua mkono, naam, na utosi wa kichwa” wa utawala wa Rumi, ambayo wilaya yake “akajichagulia sehemu ya kwanza, kwani ndiko lilikowekwa fungu la mtoa-sheria.” Kwa Gadi “akaja pamoja wakuu wa watu” kama vile wanawafanyia Jeneva. Hakuna taifa lo lote linalofaa kikamilifu maelezo ya taifa la vikosi.

13. Asheri “chakula chake kitakuwa kinono, naye atatoa tunu za kifalme” (Mwa. 49:20). Maelezo haya ya kipekee yanatoa kumbukumbu ya Ubelgiji pekee na jamaa yake Lusembagi. Kutoka Ubelgiji unapatikana uchoraji mzuri, urembo wa kifalme ambao ulipamba ukumbi wa wafalme, almasi iliyochongwa vizuri, karure na lesi ya Ubelgiji. Ubelgiji na Lusembagi wamebarikiwa zaidi ya wana wengine wa Yakobo “ Na abarikiwe

Asheri kwa watoto;na akubaliwe katika nduguze,na achovyo mguu wake katika mafuta” ya mafanikio.Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba;na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.Kwa sababu ya madini ya urani,mafanikio ya Ubelgiji yataendelea kukua.(Vile Kumbukumu 33:25 kinatoa hapo juu ni sahihi lakini haieleweki vizuri.)

**MUHTASARI:**Hapa tunayo marudio kwa muhtasari ya unabii wa Yakobo wa siku za mwisho,na baraka za Musa (zingine zinaashiria millennia).ULIMWENGUNI KOTE HAKUNA KIKUNDI CHA MATAIFA KINACHOHUSIANA NA UNABII KIKAMILIFU.Na ndani ya kikundi cha kipekee cha mataifa hiki,kila taifa lina sifa zake.(LOCATION OF THE TRIBES OF ISRAEL by Herman L Hoeh(ca. 1950s)<http://www.giveshare.org/israel/locationstribes.html>)

Kuhusiana na Gadi, wacha niongeze maandiko yafuatayo:

20 Na Gadi akamnena, “Na abarikiwe amwongezaye Gadi;Yeye hukaa kama simba mke,Hurarua mkono,naam,na utosi wa kichwa.21 Akajichagulia sehemu ya kwanza,Kwani ndiko lililowekwa fungu la mtoa-sheria;Akaja pamoja na wakuu wa watu,Akaitekeleza haki ya BWANA,Na hukumu zake kwa Israeli.” (Kumbukumbu la Torati 33:20-21).

Uswizi,hasa Jeneva,imekuwa na historia ya kuwa “mtoa-sheria wa kimataifa.”Kumbuka:Hata kama uhamiaji wa babu zetu wengine wa Uswizi na Ujerumani wanafanana,wakati wengine wamefundisha kimakosa kwamba Ujerumani ni Gadi,Ujerumani kama nchi haina historia ya kuwa mtoa-sheria inayojulikana-lakini kimsingi wametoka kwa ukoo wa Ashuru.

Haya ni maelezo zaidi ya makabila mengine,moja kwa moja kutoka kwa Biblia:

6 Reubeni ni aishi,asife;lakini watu wake na wawe wachache.

7 Na baraka ya Yuda ni hii;akasema,Isikize,Ee BWANA,sauti ya Yuda,umlete ndani kwa watu wake;alijitetea kwa mikono yake;Nawe utakuwa msaada juu ya adui zake.

8 Akamnena Lawi,Thumimu yako na Urimu yako vina mtakatifu wako,Uliyemjaribu huko Masa;ukaleta naye kwenye maji ya Meriba.9 Aliyemtaja baba yake,Mimi sikumwona;Wala nduguze hakuwakubali;Wala hukuwajua watoto wake mwenyewe;Maana wameliangalia neno lako,wamelishika agano lako.10 Watamfundisha Yakobo hukumu zako,Na Israeli torati yako,wataweka uvumba mbele zako,Na sadaka nzima za kuteketezwa madhabahuni mwako.11 Ee BWANA,ubariki mali zake,Utakabali kazi ya mikono yake,uwapige viuno vya vyao waondokao juu yake,Na wenye kumchukia,wasiinuke tena.

12 Akamnena Benyamini,Mpenzi wa BWANA atakaa salama kwake;Yuamfunika mchana kutwa,Naye hukaa kati ya mabega yake.” (Kumukumbu la Torati 33:6-12)

18 Na Zabuloni akamnena,Furahi Zabuloni,katika kutoka kwako;19 Watayaita mataifa waje mlimani;Wakasongeze huko sadaka za haki;Kwa kuwa watanyonya wingi wa bahari,Na akiba zilizofichamana za mchangani. (Kumbukumbu la Torati 33:18-19)

22 Na Dani akamnena, Dani ni mwana-simba, arukaye kutoka Bashani.

23 Na Naftali akamnena, Ee Naftali, uliyeshiba fadhili, Uliyejawa na baraka ya BWANA; Umiliki magharibi na kusini.

24 Na Asheri akamnena, Na abarikiwe Asheri kwa watoto; Na akubaliwe katika nduguze, Na aachovye mguu wake katika mafuta. 25 Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako. (Kumbukumbu la Torati 33:22-25)

Ni ya muhimu kutambua kwamba neno "magharibi" lililotafsiriwa kuhusu Naftali pia linaweza kufafanuliwa kama bahari ingurumayo, vile Herman Hoeh alivyoeleza. Uswidi inapatikana kwenye mpaka wa magharibi ya Bahari ya Baltiki.

Ingawa "wanathiolojia" wengine wamekana dhana kwamba Israeli ni tofauti na Yuda, Biblia imeeleza kauli hiyo hadi siku za mwisho (Ufunuo 18:2-5) kwamba kutakuwako na tofauti kati ya mataifa hayo mawili:

5 Kwa maana Israeli, wala Yuda, hakuachwa na Mungu wake, BWANA wa majeshi; ijapokuwa nchi yao imejaa hatia juu yake aliye Mtakatifu wa Israeli. 6 Kimbieni kutika kati ya Babeli, kila mtu na ajiokoe nafsi yake; msikataliwe mbali katika uovu wake; maana ni wakati wa kisasi cha BWANA, atamlipa malipo. (Yeremia 51:5-6)

Kwa hivyo, licha ya wakosoaji, wanaoamini Biblia wanagundua kwamba Mungu anazingatia kwamba Israeli (wanaoitwa makabila kumi waliyopotea) na Yuda (Yuda, Lawi, na pengine sehemu

ya Benyamini) bado wapo na wanaishi maeneo tofauti.

Kabla sijaenda mbali, pengine inafaa nitaje kwamba kuna unabii mwingi unaohusu taifa liitwalo Israeli leo (ambalo limetoka kwa Yuda) ambao unafaa utajwe:

20 Lakini, hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia. (Luka 21:20)

15 Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu), 16 ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani. (Mathayo 24:15-16)

22 Sauti imesikiwa, Tazama, inakuja; mshind o mkuu kutoka nchi ya kaskazini, ili kuifanya miji ya Yuda kuwa ukiwa, makao ya mbweha. (Yeremia 10:22)

6 tena watoto wa Yuda na watoto wa Yerusalemu mmewauzia Wayunani, mpate kuwahamisha mbali na mipaka yao. (Yoeli 3:6)

Janga limetabiriwa kwa taifa linalojulikana leo kama Israeli (Isaya 22:7-10). Na wakaazi watakaosalia watakuwa watumwa, na wilaya yake itatawaliwa na watu wa magharibi, kama Wagiriki (Kumbuka: utawala wa zamani wa Ugiriki uliunda utawala mwingi wa Rumi wa kizamani, kwa hivyo wilaya tofauti na Ugiriki inaweza kuwa kama ya Israeli ya kisasa).

Pengine inafaa itajwe pia kwamba Yesu alieleza waziwazi kwamba makabila kumi na mawili watakuwepo hadi mwisho:

24 Yakatokea mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa. 25 Akawaambia, Wafalme wa Mataifa huwatawala, ma wenye mamlaka juu yao huitwa wenye fadhili, 26 lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama Yule atumikaye. 27 Maana aliye mkubwa ni yupi? Yeye aketiye chakulani? Lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye. Nanyi ndinyi mlidumu pamoja name katika majaribu yangu. 29 Nami nawawekea ninyi ufalme, kama vile Baba yangu alivyoniwekea mimi; 30 mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu; na kuketi katika viti vya enzi, huku mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli. (Luka 22:24-30)

Kumbuka pia:

14 Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana-Kondoo. 15 Na yeye aliyesema nami alikuwa na mwanzi wa dhahabu, apate kuupima huo mji, na milango yake, na ukuta wake. 16 Na ule mji ni wa mraba, na marefu yake sawasawa na mapana yake. Akaupima mji wa ule mwanzi; ulikuwa kama maili elfu na mia tano; marefu yake na mapana yake na kwenda juu kwake ni sawasawa. 17 Akaupima ukuta wake ukapata dhira mia na arobaini na nne, kwa kipimo cha kibinadamu, maana yake, cha malaika. 18 Na majenzi ya ule ukuta wake yalikuwa ya yaspi, na mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kioo safi. 19 Na msingi wa ukuta wa mji ilikuwa imepambwa kwa vito vya thamani vya kila namna. Msingi wa kwanza

ulikuwa yaspi; wa pili yakuti samawi; wa tatu kalkedoni; wan ne zumaridi; 20 wa tano sardonio; wa sita akiki; wa saba krisolithi; wa nane zabarajadi; wa kenda yakuti ya manjano; wa kumi krisopraso; wa kumi na moja haikintho; wa kumi na mbili amethisto. 21 Na ile milango kumi na miwili ni lulu kumi na mbili; kila mlango ni lulu moja. Na njia ya mji ni dhahabu safi kama kioo kianguvu. (Ufunuo 21:14-21)

Basi, Mungu ana mpango na makabila kumi na mbili kulinganana na Agano Jipya. Mitume watatawala makabila kumi na mbili.

#### **Unabii Mwingi wa Agano Jipya Kuhusu Ukoo wa Yakobo haujatimika**

Na wakati wachambuzi wengi wanaelewa mafungu kutoka kwa Yakobo katika Mwanzo 48 na 49 kuwa ni unabii, wengi wanaonekana wanakubali kwamba unabii umetimika zamani sana. Tazama alichandika mwanathiolojia wa Protestani aliyejulikana John F. Walvoord:

Kwa ujumla, unabii ambao Yakobo aliuwekea watoto wake umetimika katika historia yao iliyofuatana (Walvoord, John F. The Prophecy Handbook. Victor Books, Wheaton (IL), 1990, p.33).

Maelezo hayo yaliyo juu ni kosa la kikatili. Waprotestani wengi hawaelewi mahali Marekani imetajwa katika unabii (mengi kuhusu Marekani yanatarajiwa katika makala zijazo, lakini kwa wakati huu kumbuka Danieli 11:39 ni unabii kwamba nchi imilikayo nguvu nyingi za kijeshi itatokomezwa katika nyakati za mwisho na Habakuki 2:6-8 inaonyesha kuondolewa kwa watu walio na deni kubwa).

Siyu kwamba unabii mwingi haujatimika kihistoria, lakini unabii mwingi ulikuwa wa siku za mwisho.

Ilikuwa wakati wa Agano Jipya ambapo siku za mwisho zilianza. (Waebrania 1:2),,na hakuna mchambuzi (nje ya wale wanaokubali kwamba bado kuna makabila ya Israeli wanaoshirikiana na taifa linaloitwa Israeli leo) ambaye ameweza kuonyesha jinsi unabii wa Mwanzo 49:1-27 umetimika katika “siku za mwisho.” Ama sijomwona ye yote kati yao anayeeleza “kundi la mataifa” ni nani ambao wangetoka kwa ukoo wa Efraimu.

Kwa upande mwingine, hayati John Ogwyn aliandika:

Hamna rekodi ya Efraimu na Manase kuwa taifa kuu na kundi la mataifa kabla ya utekaji wa Israeli.Hawakuwa baraka kwa mataifa yote ya ulimwengu kabla ya kuenda kwa utekaji wa Ashuru mnamo karne ya kumi na nane kabla ya Kristo.Kwa hakika, utimizaji wa ahadi ambayo Mungu alimpa Abrahamu na kuthibitisha tena kwa ukoo wake haikuwepo mpaka makabila kumi kupotea kutoka kwa kurasa za Biblia yako na baadaye kutoka kwa kurasa za historia za kawaida. (Ogwyn J. 2006)

Wakati “kupotea” ndivyo wengi wanatazama, ukweli ni kwamba walitimiza unabii na wana unabii mwingi wa kutimiza.

Zaidi ya hayo, fungu moja kuu katika Biblia, baada ya lile la Mwanzo linapatikana katika Walawi 26. Kwa kawaida linaweza kuitwa fungu kuu la kwanza la “baraka na laana” katika Biblia.Bila kuenda kwa undani sana, tazama mstari mmoja:

33 Nanyi nitawatapanya-tapanya katika mataifa, name nitaufuta upanga nyuma yenu; na nchi yenu itakuwa ni ukiwa, na miji yenu maganjo. (Walawi 26:33).

Na wakati Mungu hakuwaruhusu Waashuru kutapanya watoto wa Israeli katika Agano la Kale, hawakuharibu miji yao. Badala yake miji ilibaki na Waashuru waliweka watu wengine katika miji hiyo (2 Wafalme 17:24).

Na kwa nini hii inafaa?

Kwa sababu unabii ambao unasema “miji” itakuwa “maganjo” bado unangoja utimike.Basi,huu ni unabii wa Agano la Kale ambao utafanyika-na kuna uwezekano kwamba utaathiri Efraimu na Manase.Efraimu na Manase wanaitwa “watu wakuu” katika Biblia (Yoshua 17:17).

Ya ajabu ni kwamba Biblia katika sehemu zingine inatofautisha kati ya ukoo wa Yuda na ule wa Yusufu.Kumbuka sehemu moja hiyo:

Na wewe mwanadamu,twaa kijiti kimoja;ukaandike juu yake,Kwa Yuda,na kwa wana wa Israeli wenzake;kasha,twaa kijiti cha pili ukaandike juu yake,Kwa Yusufu,kijiti cha Efraimu,na kwa nyumba yote ya Israeli wenzake; (Ezekieli 37:16).

Vile vile kumbuka:

3 Ninyi mnaoiweka mbali siku hiyo mbaya,na kulileta karibu kao la udhalimu...6 ninyi mnaokunywa divai katika mabakuli,na kujipakia marhamu iliyo nzuri;lakini hawahuzuniki kwa sababu ya mateso ya Yusufu.7 Basi kwa ajili ya hayo sasa watakwenda utumwani pamoja na wa kwanza watakaokwenda utumwani,na kelele za machezo za hao waliojinyosha zitakoma.8 Bwana MUNGU ameapa kwa nafsi yake,asema BWANA,MUNGU WA MAJESHI;Naizira fahari ya Yakobo,nachukizwa na majumba yake;kwa sababu hiyo nitautoa



huo mji, pamoja na wote waliomo ndani yake (Amosi 6:3,6-8).

Ukoo wa Yusufu, ambao pia unajulikana kama Yakobo, wataadhibiwa (Yeremia 30:7) kwa dhambi yao pamoja na majivuno. Kumbuka kwamba wanafikiria haitafanyika kwao lakini itafanyika:

8 Angalieni, macho ya Bwana MUNGU yanaungalia ufalme wenye dhambi, name nitaungamiza utoke juu ya uso wa dunia; lakini sitaingamiza kabisa nyumba ya Yakobo, asema BWANA. 9 Kwa maana, angalieni, nitatoa amri, name nitaipepete nyumba ya Israeli katika mataifa yote, kama vile ngano ipepetwavyo katika ungo lakini hata chembe moja iliyo ndogo haitaanguka chini. 10 Wenye dhambi wote katika watu wangu watakufa kwa upanga, hao wasema Mabaya hayatatupata nyuma wala mbele. (Amosi 9:8-10)

Je, mataifa ya Marekani na washiriki wake wazungu ni wenye dhambi? Biblia inaonyesha kwamba ukoo wa Yakobo na Yusufu ni watu wa Mungu (Zaburi 77:15). Na kwa sababu Mungu atawapepete nje, Anawajua ni kina nani!

Pia kumbuka unabii ufuatao:

25 "Kwa sababu hiyo, Bwana MUNGU asema hivi, Sasa nitawarejeza watu wa Yakobo waliohamishwa, nitawahurumia nyumba yote ya Israeli; nami nitalionea wivu jina langu takatifu. 26 Nao watachukua aibu yao, na makosa yao yote waliyoniasi, watakapokaa salama katika nchi yao wenye, wala hapana mtu atakayewatia hofu; 27 nitakapokuwa nitakapowaleta tena kutoka kabila za watu, na kuwakusanya kwa kuwatoa katika kchi ya adui zao, na kutakaswa kati yao mbele ya macho ya mataifa mengi. 28 Nao watajua ya

kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wao, kwa kuwa naliwahamisha, waende utumwani kati ya mataifa, na mimi nitawakusanya, na kuwaingiza katika nchi yao wenyewe; wala sitawaacha tena huko kamwe, hata mmojawapo; 29 wala sitawaficha uso wangu tena; kwa maana nimemwaga roho yangu juu ya nyumba ya Israeli, asema Bwana MUNGU. (Ezekieli 39:25-29)

Huu haukutimizwa na Wayahudi wanaorudi kwa nchi yao inayopatikana Mashariki ya Kati na kuunda taifa la Israeli mwaka wa 1948. Kwa nini? Kwa sababu Wayahudi wengi walikuwa watu wa dunia wakati huo na wakati huu. Wote HAWAJUI Mungu aliye hai-ambaye unabii unaonyesha kwamba watamjua, na bado haujatimika.

Na je wale ambao hawajatoka kwa ukoo wa Yuda, Efraimu ama Manase? Makabila mengine yaliosalia? Vizuri, wakati mateso ya Yakobo (Yeremia 30:7) hautaanza na adhabu pamoja (Ezekieli 5:1-3 inaonekana inaashiria Yuda, Efraimu na Manase), wao pia watapokea adhabu (tazama herufi nzito katika mwisho wa mstari 4):

1 Nawe, mwanadamu, ujipatie upanga mkali, kama wembe wa kinyozi ujipatie, ukaupitisha juu ya kichwa chako na ndevu zako; kasha ujipatie mizani ya kupimia, ukazigawanye nywele hizo. 2 Theluthi ya hizo utaiteteza katikati ya mji, siku za mazingiwa zitakapotimia; nawe utatwaa theluthi, na kuipiga kwa upanga pande zote; nawe utatawanya theluthi ichukuliwe na upepo, name nitafuta upanga nyuma yake. 4 Nawe utatwaa tena baadhi ya hizo, na kuzitupa katikati ya moto na kuziteketeza katika moto huo; kutoka nywele hizo moto utakuja na kuingia


**katika nyumba yote ya Israeli.**  
(Ezekieli 5:1-4)

Sehemu iliyowekwa herufi nzito inaonekana kuonyesha kwamba nyumba ya Israeli yote itakuwa na dhiki baada ya taifa la kisasa ambalo ni Israeli na nchi za wazungu zitaenda. Hizi ni nchi kama Ufaransa, Ufini, Uholanzi, Uswisi, Denmaki, Irelandi, Ubelgiji, Lusembagi, Uswidi na Norwei. "Idadi hii ndogo" katika mstari wa 3 inaonekana kuwa ni asilimia 10 kwa sababu hiyo ndiyo idadi Isaya 6:13 inaonyesha itabaki. Kama vile Ezekieli 5:4 inaonyesha, baada ya Marekani kuondolewa, moto utawaka kwa "nyumba yote ya Israeli."

(Wengine wameuliza kama mataifa yaliyotoka kwa Israeli yanawezakuwa sehemu ya utawala wa Mnyama wa mwisho. Historia inatonyesha kwamba Ufaransa, Uswisi, na sehemu ya Uholanzi kidogo, Lusembagi, Ubelgiji, na Uingereza zilikuwa sehemu za Utawala wa Rumi wa zamani. Sehemu ndogo ya Ufaransa, na pia Uholanzi mzima, Lusembagi, Uswisi na Ubelgiji zilikuwa sehemu iliyoitwa "Utawala Mtakatifu wa Rumi." Zingatia pia kwamba washiriki watatu wa nyumba ya Lusembagi walitawala kama "Watawala wa Rumi Mtakatifu." Ukweli ni kwamba angalau sehemu ya Waisraeli walikuwa sehemu ya mnyama wa Danieli 2:40-43 na 7:2-8, inafaa ionyeshe kwa jumla, kwa wakati, inawezakuwa utawala wa mwisho wa Mnyama.)

Kwa ukweli, baada ya Yesu kurudi na kuunda Ufalme wake, adhabu zote za aina hizo zitaisha. Lakini kabla ya wakati huo, wakati wa dhiki utaangukia ukoo wa Israeli-lakini wote hawataharibiwa kwa sababu wengine wataokolewa (Yeremia 30:7).

**Vidokezi Ishirini na Nane vya Maombi Yanayofaa: Sehemu ya 7**



*Kijitabu cha Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG) cha maombi*

Na Bob Thiel

Hii ni sehemu ya saba ya sehemu nyingi mfululizo kuhusu maombi.

Imesemekana kwamba, "Kanisa la Mungu linaenda mbele kwa kupiga magoti. "Msemo huu umekuwa ukitumika kama himizo kuwaambia Wakristo kwamba wanapaswa kuomba. Lakini kwa namna gani?

Katika makala iliyopita, maombi yalifafanuliwa, na vidokezi ishirini na moja. Katika makala hii vidokezi vingine vitatu, kuanzia na kile tunachoita kidokezi ishirini na sita kimejadiliwa pamoja na muhtasari wa vidokezi vyote ishirini na nane.

**Kidokezi 26:Kabiliana na "Dhambi za Siri"**

Wakati mwingine una dhambi ambazo ziko njiani, pamoja na siri. Mungu hatakusikia ukikubali maovu:

18 Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia (Zaburi 66:18).

1 Tazama, mkono wa BWANA haukupunguka hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; 2 lakini

maovu yenu yamewafarakisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone hata hataki kusikia (Isaya 59:1-2).

Wengine wanafanya kazi mzuri ya kuzificha dhambi zao zisijulikane na wengine. Wengine hata wanaficha dhambi zao wasijue. Lakini anajua:

5 Ee Mungu unajua upumbavu wangu, Wala hukufichwa dhambi yangu. (Zaburi 69:5)

7 Maana tumewatoweshwa kwa hasira yako, Na kwa ghadhabu yako tumefadhaishwa 8 Umeyaweka maovu yetu mbele zako, Siri zetu zote zimepita katika hasira yako, Tumetoweshwa miaka yetu kama kite. (Zaburi 90:7-8)

Mungu atakuruhusu ukubaliane na majaribu akuondolee na kukusafisha dhambi zako:

2 Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; 3 Mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. 4 Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno. (Yakobo 1:2-4)

Lazima tufanye bidii ili tuwe wakamilifu mbele ya Mungu, siyo mbele yetu. Yesu alifundisha:

48 Basi ninyi mtakuwa wakamilifu kama baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. (Mathayo 5:48)

Hatuwezi kuzificha dhambi zetu mbele ya Mungu na inafaa tufanye bidii tusijifiche dhambi zetu.

Kumbuka vile Agano Jipya na Kale yanafundisha:

39 Mbona anung'unika mwanadamu aliye hai, Mtu akiadhibiwa kwa dhambi zake? 40 Na tuchunguze njia zetu na kuzijaribu, Na kumrudia BWANA tena 41 Na tumwinulie Mungu aliye mbinguni mioyo yetu na mikono. (Maombolezo 3:39-41)

27 Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mewili na damu ya Bwana. 28 alakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule na kukinywea kikombe. 29 Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. 30 Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi ma dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala. 31 Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa 32 ili tuhukumiwapo twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia. (1 Wakorintho 11:27-32)

Lakini wanadamu huwa hawaamini jambo hilo. Tunafikiri shida zetu ni za kimwili na zinahitaji suluhisho la kimwili, wakati shida nyingi ni za kiroho na zinahitaji suluhisho la kiroho. Hya hayamaanishi kwamba tupuuzie za kimwili, lakini elewa pia kiroho:

7 Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche BWANA, ukajiepushe na uovu. 8 Itakuwa afya mwilini pake, Na mafuta mifupani mwako. (Mithali 3:7-8).

2 Kwa nini kutumia fedha kwa kitu ambacho si chakula, na kutabikia kitu kisichoshibisha? Sikilizeni, nisikilizeni mimi na mle kilicho kizuri, nazo nafsi zenu zitafurahia utajiri wa unono. 3 Tegeni sikio mje kwangu, nisikie mimi, ili nafsi

zenu zipate kuishi. Nitafanya Agano la milele nanyi, pendo la uaminifu nililomwahidi Daudi. (Isaya 55:2-3)

12 Na karibu na mto, juu ya ukingo wake, upnade huu na upande huu, utamea kila mti wa chakula, ambao majani yake hayatanyauka, wala matunda yake hayatatindika kamwe; utatoa matunda mapya kila mwezi, kwa sababu maji yake yanatoka mahali patakatifu, na matunda yake yatakuwa ni chakula; na majani yake yatakuwa ni dawa. (Ezekieli 47:12)

7 Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae; nawe ujioze kupata utauwa. 8 Kwa maana kujiozea kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwepo baadaye. 9 Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa; 10 Kwa maana twajitaabisha na kutahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote hasa wa waaminio. 11 Mambo haya uyaagize na kuyafundisha. (1 Timotheo 4:7-11)

Jichunguze na ubadilike. Kumbuka Biblia inafundisha:

12 Kwa hiyo anayedhani kuwa amesimama na aangalie asianguke. (1 Wakorintho 10:12)

Sisi sote twahitaji imani zaidi na subira. Yesu hata aliuliza kama arudipo atapata imani duniani:

8 Nawaambia atawapatia haki upesi; walakini, atakapokuja Mwana wa Adamu, ije! Ataiona imani duniani? (Luka 18:8).

Yesu alitabiri kwamba kutakuwako na shida ya imani nyakati za mwisho. Sote tunahitaji imani zaidi, sote twahitaji kudadilika.

### **Kidokezi 27: Mabadiliko Yawezafanya Lisilowezezana Liwezekane**

Je, itakuwaje kama unayopitia inaonekane haiwezekani?

Kulingana na Biblia hakuna lisilowezezana:

13 Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. (1 Wakorintho 10:13)

Kumbuka kumpinga shetani wakati wa mitihani na majaribu, na Mungu atakutengenezea njia na utashinda. Geuza matukio ya uharibifu yawe matukio ya kujenga tabia zako.

Vipengele kama kupunguza mizani na kuacha kuvuta sigara ni ngumu lakini vinawezezana. Vipengele kama mtu mzima kukua futi 1 1/2 (Mathayo 6:27) ama aliyezaliwa kipofu kupata kuona bila kuingilia kati kwa njia ya matibabu (Yohana 9:30-33 kimsingi haviwezekani. Wakati mwingine tunakabiliana na lisiliwezekana, kwa sababu Mungu anaamini tunaweza kushughulikia na inaweza kutusaidia kujenga tabia zetu. Wakati mwingine, pengine inatutia moyo ili tuwe karibu na Mungu.

Mitihani na majaribu mengine yanapaswa kuchukuliwa moja kwa wakati mmoja. Usijiuze kama mbilikimo. Kwa sababu karibu kila kitu unaweza kutatua kwa siku ingine. Usisumbuke na kujiambia kwamba huwezi kuendelea. Kumbuka kwamba Yesu alifundisha kwamba:

31 Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au tunywe nini? Au

tuvae nini? 32 Kwa maana hayo yote Mtaifa huyatafuta ; kwa sababu Baba yenu wangu wa mbinguni anajua kuwa mnahitaji hayo yote. 33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake : na hayo yote mtazidishiwa. 34 Basi msisumbukie ya kesho ; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatesha kwa siku maovu yake. (Mathayo 6 :31-34)

Majaribu mengi yanafaa yatatuliwe kila moja kwa wakati wako jinsi Yesu alivyonena hapo juu.

Tunafaa pia tujihadhari kuhusu kujilinganisha na wengine:

12 Kwa kuwa hatuthubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe, wala kujilinganisha nao ; bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao na nafsi zao, hawana akili. (2 Wakorintho 10 : 12)

Kwa nini majaribu mengine ya Wakristo yanaonekana magumu kuliko walioko nje?

17 Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu;na ikianza kwetu sisi,mwisho wao wasiotii injili ya Mungu utakuwaje? 18 Na mwenye haki akiokoka kwa shida,Yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi? 19 Basi wao wateswao kwa mapenzi ya Mungu na wamwekee amana roho zao,katika kutenda mema,kama kwa Mungu mwaminifu.(1 Petro 4:17-19)

Kwa hivyo,Wakristo wanaweza kupata wanapambana na maswala ambayo wengine hawapati.Licha ya shida,lazima tujaribu kufanya mema,hata wakati wa shida.

Kama vile suala la maombi linavyoenda,je ikiwa unachotaka hakiwezekani?

Basi,kulingana na Mungu,hakuna lisilowezekana:

26 Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; Bali kwa Mungu yote yawezekana. (Mathayo 26:19)

23 Yesu akawaambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye. (Mariko 9:23)

36 Akasema, Aba, Baba, yote yawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki, walakini; si nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe. (Mariko 14:36)

Unaweza kusema kwamba ni vyema kwa Mungu, lakini mimi ni mdhaifu kwa hivyo lisilowezekana haliwezi kunitokea. Haya, je, umeamini kweli yanayosemwa na Biblia:

13 Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.(Wafilipi 4:13)

Unaweza kusema, “Sawa hiyo ilikuwa ukweli kwa Mtume Paulo.Paulo alikuwa mtu mkuu wa imani.Lakini mimi si kitu.Nimetenda dhambi sana.”

Sawa, kumbuka kwamba Mtume Paulo awali “aliudhi Kanisa la Mungu kupita kiasi” (Wagalatia 1:13). Wewe wakati mwingine haujatenda maovu kiasi hicho. Hata kama ulifanya, bado unaweza kutubu.

Lakini hoja kamili ni kwamba,kupitia kwa Kristo,Wafuasi wake wanaweza kufanya kila kitu.

Hata kuponya wagonjwa:

2 Eeh nafsi yangu, umhimidi BWANA. Naam vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu.

3 Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, Wala usizisahau fadhili zake zote. 4 Aukomboha uhai wako na kaburi, Akutia taji taji ya fadhili na rehema, 5 Aushibisha mema uzee wako, ujana wako ukarejezwa kama tai; 6 BWANA ndiye afanyaye mambo ya haki, na hukumu kwa wote wanaoonewa. 7 Alimjulisha Musa njia zake, wana wa Israeli matendo yake. 8 BWANA amejaa huruma na neema, Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili. 9 Yeye hatateta sikuzote, wala hatashika hasira yake milele. 10 Hakututenda sawasawa na hatia zetu, wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu. 11 Maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, Kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. 12 Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi. (Zaburi 103:1-12)

Lakini huenda ukasema, wewe au mwingine uliyemwombea hajapona.

Wakati Mungu anayaponya magonjwa yote, anaifanya tu wakati amehisi uponyaji utamsaidia kwa ukweli anayeugua.

Wakati mwingine si dhahiri kwa nini hupati unalohitaji ama unalosihi ulipate. Je, hii ni lazima kwa sababu umekosa imani?

Hapana.

Kumbuka kilichofanyika kwa Mtume Paulo ambaye aliandika:

7 Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige nisije nikajivuna kupita kiasi. 8 kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. 9 Naye akaniambia, Neema yangu

yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu wngu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. 10 Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo nguvu. (2 Wakorintho 12:7-10)

Kwa nini Mungu hakumponya Mtume Paulo?

Kwa sababu ingemwathiri Paulo kwa njia mbaya. Fungu hilo la juu linaonyesha kwamba Paulo na/ama watu waliokuwa karibu naye hawangeweza kushughulikia masuala vizuri kama Paulo hangekuwa na udhaifu. Ama pengine kwa sababu Paulo alikuwa na tabia ya kuvumilia na akawa kama kielelezo, kwa hivyo Mungu akaamua kuwa udhaifu wake ulikuwa bora zaidi.

Paulo pengine alihisi kwamba angefanya kazi ya Mungu vizuri ikiwa Mungu angeponya kwa udhaifu wowote. Kwa sababu ya maelezo katika Wagalatia 4:15 na 6:11, wengine wanahisi kwamba matatizo haya yangukuwa ni ya macho. Ikiwa ni hivyo, kumbuka kwamba kwa sababu Paulo aliandika vitabu vingi vya Agano Jipya kuliko kila mtu, Mungu hangehitaji Paulo apate kuponywa, hata kama Paulo angefikiria nini. Hata maombi ya Paulo hayangeponya kila mtu aliyemwombea. Paulo ametaja shida ya tumbo iliyomsumbua Timotheo kila wakati katika 1 Timotheo 5:23, na pia akasema, "Trofimo nalimwacha huko Melito, hawezi. (2 Timotheo 4:20)

Kujenga tabia ni muhimu sana kwa Mungu, na mapenzi ya Mungu, kuliko uponyaji wa kimwili. Hiyo haimanishi kwamba "kisichowezekani" hakitafanywa. Bado, uzoefu wa Mtume Paulo unasaidia kuonyesha kwamba mapenzi ya Mungu hatimaye yanashinda unachokithamini kimwili.

Unaweza kufikiri kwamba haufai mbele ya Mungu na hawezi kusikia maombi yako, lakini wote wametenda dhambi:

23...wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. (Warumi 3:23)

8 Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. 9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaniminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. 10 Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu. (1 Yohana 1:8-10)

Ukiamini na kuungama dhambi zako, Mungu atakusikia. Lakini unaweza kuwa na tabia nyingi za kukuza kwa maeneo unayoweza kuyafikiria.

#### **Kidokezi 28: Funga Maombi na Amina**

Yesu alifunga maombi aliyoomba katika Mathayo 6 na neno "Amina". Amina linatoka kwa kitenzi aman linalimaanisha "kuunga mkono, kuthibitisha, ama kumaliza" (*Harkavy, Student's Hebrew and Chaldee Dictionary*). Amina lenyewe linamaanisha "kwa ukweli" (sawa na hapo). Kristo mara nyingi alitumia neno hili katika Agano Jipya ambapo (katika King James Version) limetafsiriwa "amin." Kimsingi neno hili linaonyesha kwamba umeamini na kukubali na yaliyosemwa awali.

Amini ulichokiomba. Uwe na mtazamo mzuri. Amina.

#### **Muhtasari**

Basi hii ni orodha ya vidokezi 28:

1. Omba kwa Mungu Baba
2. Abudu Mungu kwa ukweli

3. Mtii Mungu. Fanya zaidi ya mapepo
4. Abudu Mungu kwa roho
5. Amini Mungu
6. Mpinge Shetani
7. Usipigane na Mungu
8. Waombee wengine
9. Ombea mahitaji yako
10. Kumbuka mapenzi ya Mungu na uvipange vipaumbele vyako.
11. Msimamo wako wakati wa Maombi kutoka kwa Biblia.
12. Omba kila siku
13. Msamaha.
14. Tambua Roho wa Mungu
15. Omba kwa kile ambacho Biblia kinasema ukiombee
16. Omba karama za Roho
17. Usiombe ili uonekane
18. Umtii kufunika kwa kichwa kulingana na Agano Jipya
19. Omba kila mara, usipayuke payuke, lakini uwe na bidii.
20. Ikiwa unateseka, ama umegonjeka, omba
21. Waombee viongozi wa Kanisa
22. Waombee viongozi wa serikali
23. Weka Yesu katika maombi yako
24. Mambo magumu: Kumbuka kufunga
25. Omba na kushukuru
26. Kabiliana na 'dhambi za siri'



**27. Mabadiliko yawezafanya  
lisilowezezana liwezekane**

**28. Funga maombi na Amina.**

Wengine wanaweza kufikiri:

“Ngojea kwanza! Nataka Mungu afanye vitu NINAVYOTAKA. Hii ndiyo maana naomba. Na unaendelea kuyataja maandiko kwamba ninahitaji kuungama dhambi zangu, niombee wengine, niombee kazi yake, niombee mapenzi ya Mungu yafanyike, nimshukuru, na hata kufunga. Hivyo si vidokezi nilikuwa natumai.”

Sawa, unaweza kumwamini Mungu wa Biblia ama usimwamini. Unaweza ukaombea mahitaji yako, lakini inafaa uelewe kwamba maombi yanakusudiwa kuzidi mchakato wa “tafadhali nipe hii, tafadhali nipe ile.”

Soma, rudia na ujitahidi kuelewa vidokezi vyote katika kijitabu hiki. Soma Biblia. Omba kila mara kwa Mungu Baba.

Ikiwa utaamini na utafuata yanayosemwa na Biblia, Mungu atajibu maombi yako. Vidokezi ishirini na nane katika kijitabu hiki vinafaa kukupa angalau kianzio cha kugundua jinsi Mungu anataka utazame maombi.

17 Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi. (Yakobo 4:17)

**Omba.**

**Maelezo mengi kuhusu maombi yanapatikana katika kijitabu chetu cha**  
**Maombi: Biblia inafundisha**

**Nini?**

**KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA**

**Somo 12a: Thibitisho la Historia ya Biblia-utangulizi**



Bob Thiel, Mhariri Mkuu

Imechapishwa 2017 na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)

Kozi hii imetokana kwa kiwango kikubwa na kozi kwa Mawasiliano iliyohaririwa mwaka 1954. Iliyoanza chini ya usimamizi wa hayati C. Paul Meredith kupitia Kanisa la Mungu la Redio. Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebaki yalivyo). Kadhalika imeongezewa vifungu toka Maandiko Matakatifu, pamoja na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali.

**Kumbuka:** Somo hili lilikuwa refu hapo awali, ilihitajika ligawanywe katika visehemu vingi kwa vile lilikuwa refu kuliko kiwango cha toleo la jarida hili. Sehemu ingine, 12 b, imepangwa kwenye toleo la jarida litakalofuata hili.

**HISTORIA NA AKIOLOJIA ZINATHIBITISHA UKWELI WA BIBLIA**

Je, KUNA uthibitisho NJE ya Biblia kwamba matukio yaliyoelezwa kwenye maandiko yalifanyika-kwamba wahusika wake wakuu walipata kuhishi?

Wapi thibitisho kwamba Yusufu alihishi Misri? -kwamba Ibrahimu na mababu zake walikuwepo? -kwamba kwa hakika Daudi alikuwa mfalme wa Israeli? -na, zaidi ya yote, kwamba Kristo na mitume walijulikana na Wayahudi na watu wa mataifa walioishi wakati huo?

Na wapi THIBITISHO kwamba Neno la Mungu takatifu lilihifadhiwa kisahihili ili tutumie leo hii-haswa vile kuna tafsiri nyingi tofauti za kisasa?

Ndiyo, WAPI THIBITISHO?

Ni wakati wa kusoma thibitisho la HISTORIA na AKIOLOJIA ili tuthibitishwe zaidi kuwa Biblia ni UKWELI, na siyo hekaya.

#### **Wahudumu Wanakana Asili Takatifu**

Pengine ITAKUSTUA kujua vile viongozi wengi wa kidini wanafikiria na wanayosema wazi kuhusu Biblia! Hapa ni kile alichandika Harry Emerson Fosdick, Mhudumu wa Marekani aliyejulikana, katika kitabu chake, "Matumizi ya kisasa ya Biblia":

" Tunajua sasa kwamba kila wazo katika Biblia lilianza kwa njia isiyo ya kistaarabu na kwa chanzo cha kitoto..."na hili ni "jaribio lisilowezezana la kujipatanisha Biblia, kuifanya iongee kwa sauti moja, ili ipate kusuluhisha migogoro yake na ukinzani wake..." (Kurasa 11,24).

Kwa nini Dk.Fosdick aliandika hii? Je, aliridhishwa kwamba hakuna thibitisho lo lote la msukumo wa Biblia? AMA ALIKUWA AKIPUUZIA THIBITISHO-NA KUPUUZIA UKWELI?

Kwa maandiko ya awali ya Biblia, aliongezea kusema: "Lakini hatutaki kuomba msamaha kwa ubichi wao... ukosefu wao ni ukosefu wa ukomavu..."

Leo hii inashangaza kugundua kwamba viongozi wa kidini wanaamini Biblia siyo

ya kistaarabu na ni ya kitoto, ina ubichi na imekosa ukomavu-kitabu cha hekaya na hadithi badala ya UKWELI WA MUNGU uliotiwa msukumo!

#### **Wasomi wa Biblia ni Wakosoaji Pia**

Dk. James Moffat, ambaye alichapisha Biblia inayojulikana ya Kiingereza, alisema katika utangulizi wake wa Biblia kwamba vitabu vyake vingi ni "maandishi ya wanafunzi yaliyofanywa kwa karatasi ya fasihi ambayo yamehaririwa mara nyingi, wakati mwingine na wakusanyaji wacha Mungu."

Kwa msomi huyu vifungu vya awali vya Biblia vilitoka kwa "hamu ya kawaida ya kusanya mapokeo ya kale ya watu."

Ndiyo, huyu ni mmoja wa wasomi wa kwanza aliyetamka kwamba Biblia ina asili ya kawaida kutoka kwa MAPOKEO ya wanadamu! -kumaanisha kwamba haitekelezwi na UKWELI! Nini ilimfanya aamini dhana hiyo? Je, hakuwa na thibitisho ya msukumo wa maandiko? Hakika, ikiwa kulikuwako na thibitisho la kutiwa msukumo kwa Biblia, hawa wasomi hanwangepuuzia-Je, wangepuuzia? AMA WALIPATA USHAHIDI NA WAKAKANA?

Sasa soma alichandika Dk. Edgar J. Goodspeed, ambaye pia alitafsiri Biblia, alisema kuhusu maandiko katika kitabu chake, "Jinsi ya Kusoma Biblia." Alisema unapaswa kukumbuka hili kuhusu vitabu kumi na viwili vya kwanza: "Ni jaribio la kwanza la mwanadamu kuandaa elimu yake ya zamani kwa ile tunayoita mpangilio ya historia." Anapuuzia hata UWEZEKANO kwamba Mungu angeweza KUWATIA MSUKUMO watu walioandika Biblia!

Tukisoma Mwanzo, Dk. Goodspeed angetukumbusha kwamba:

"Mwanzo ni kamusi elezo kuu ya mawazo ya WAEBRANIA, na suluhisho la matatizo makubwa

ambayo yanakabiliana na mawazo ya wanadamu. Fanikio lake kuu ni kwamba iliweza kuunganisha Biblia yote kama kazi ya mtu aliye mkuu..." (p.39).

Je, unakamata kinachosemwa hapo juu? Biblia ni kazi ya MWANADAMU pekee yake-jaribio la MWANADAMU kuratibisha elimu ya kihistoria, suluhisho la Mwaebrania kwa matatizo ya kimaadili-WAKISINGIZIA kana kwamba maandiko hayo yametoka kwa aliye mtakatifu!

Huu ndio mtazamo kamili ya wasomi wengi! Biblia, kulingana na filozofia hii inayokosa mwelekeo, ni rekodi iliyotiwa msukumo na uchunguzi wa MWANADAMU ya dhana ya Mungu-siyo rekodi ILIYOTIWA MSUKUMO ya ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu, ya elimu bora mwanadamu anafaa kujua, lakini hangeweza vinginevyo kupata!

Kuhusu Amri za Mungu, Dk. Goodspeed anasema kwamba "inaendeleza sheria za kale zilizochukuliwa kutoka kwa Wakanani baada ya ushindi..." na zinaonyesha "...hatua mbalimbali za kanuni zinazokosa ustaarabu..." Kwa njia nyingine, Dk. Goodspeed anaamini kwamba binadamu anayekufa, mwenye tama za kimwili ndiye alitengeneza Amri kumi pamoja na sheria na hukumu za Mungu!

Na kwa sehemu ya Biblia inayosalia, anaamini "Kitabu cha Yohana ni hadithi ya NGANO ya ushindi wa Kaanani" na kwamba kitabu cha Ruthu "ni hadithi ILIYOTUNGWA ya Waisraeli, badala ya historia yake, na kinafaa kiwe miongoni mwa HEKAYA na HADITHI" (p.51).

### **Mwaminifu, lakini hajui?**

MATAMKO KAMA HAYA YANASHANGAZA KWA SABABU NI CHANZO CHA MAWAZO YA WANADAMU! Kwa wazo la kawaida Biblia ni kitabu tu cha hekaya na hadithi, na suluhisho kubwa ya maswali ya chanzo cha wanadamu na hatima yake.

Lakini ni THIBITISHO gani watu hawa wanalo kwa kutoa dhana kwamba Biblia iliandikwa kiulaghai na Waebrania ambao "walidai" msukumo mtakatifu kwa matamko yao tu ya kibinadamu?

Katika Biblia, Mungu anaongea kwa mamlaka na sisi kupitia kwa waandishi wake. BIBLIA, BASI, INAMILIKI MAMLAKA KUU KWENYE MAISHA YETU KWA VILE IMETOKA KWA MUUMBAJI WETU MKUU. Biblia inarudia mara mia: "BWANA asema hivi, katika maandiko, Mungu anaongea katika nafsi ya kwanza- "Mimi" na anatupatia changamoto kumjaribu ili TUTHIBITISHE kama anasema ukweli. (Isaya 44:6-9).

Bila Biblia HATUWEZI KUELEWA MASOMO YA KALE, MAANA YA WAKATI ULIOPO, NA LENGU LA WAKATI UJAO.

Maandiko, yakieleweka vizuri, YANATUPA MAANA YA BUSARA ya kuwepo kwa mwanadamu na vinavyosababisha maovu yote ya ulimwengu. Maandiko yanaeleza hakika kwa nini ulimwengu unakabiliana na vita, magonjwa na mateso.

Kuna "uonyaji" mwingi wa kidini, kisiasa na kiuchumi katika ulimwengu, lakini hakuna wote unaofikia chanzo cha shida za ulimwengu. WAZO LA MUNGU pekee ndilo kubwa la kujua majibu sahihi. Hakuna kitabu LAKINI BIBLIA YAKE ndiyo inaweza kueleza sheria zinazothibiti maisha ya mwanadamu milele na shughuli za wanadamu-SHERIA ambazo zikipuuzwa, zinaleta adhabu za magonjwa, vita na mauti.

Biblia pekee ndiyo inaweza kututoa kwenye machafuko yanayokuja!

Na bado wanadamu wanakana suluhisho lake kwamba ni za kizamani katika kipindi hiki cha maelezo ya kidigitali. Ukweli wake hawataki kuujuu. KWA NINI "BWANA ANA MASHINADANO NA MATAIFA" (Yeremia 25:31). TANGIA MWANZO WA MAISHA YA MWANADAMU, MUNGU AMEKUWA NA MABISHANO NA

WANADAMU. WANADAMU KWA ASILI YAKE AMEKATAA KUFUATA NJIA YA MUNGU YA MAISHA. Wanadamu wanafikiria kwamba njia zao ni nzuri. Wanadamu wanafikiri kwamba wanajua kumliko Mungu.

Ndiyo, “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia ya MAUTI (Mithali 14:12). Wanadamu wanaepuka kumtambua Mungu kama Kiongozi Mkuu. Watu wanaficha macho yao kutoka kwa ushahidi ulio wazi, na kutambulisha maandiko kwa njia ya uwongo kama imani potofu na mapokeo.

### **Wapi Thibitisho?**

Kila mtu leo hii anataka thibitisho! Watu wana kigae mabegani mwao, kwa kusema ukweli. Wanataka mtu wa kuwathibitishia ikiwa Biblia HAKIKA ni ukweli. Kristo alisema mwelekeo huu wa changamoto utafika upeo katika siku za mwisho wa ustaarabu wa mwanadamu-kabla mwanadamu na uvumbuzi wake wa kisayansi haujalipua uhai wote wa wanadamu (Luka 18:8; Mathayo 24:22).

Bila shaka ni vizuri tukithibitisha! Na kuna thibitisho-thibitisho la kushangaza sana-thibitisho ambalo litashangaza watu wengi ikiwa wanatheolojia wataungama kwa walimwengu! Lakini ulimwengu umekosa kujua kimakusudi.

Amini usiamini, ulimwengu TAYARI UMEJUA THIBITISHO lakini, kwa sababu wamedanganywa, hawana nia ya kukubali thibitisho. WAMEONA thibitisho, WAMEHISI thibitisho, WAMELICHIMBA, WAMESOMA na hata KULICHAPISHA!

Lakini wanadamu, wamedanganywa na itikadi za kidhana na mapokeo mapotofu ya kidini, WAMEKANA thibitisho kwa sababu hawataki kuamini na KUJISALIMISHA MAPENZI YAKE kwa Biblia.

Somo hili ya Kozi ya Biblia ni la nne kwa mfululizo linaloonyesha thibitisho la kuwepo kwa Mungu na msukumo wa ufunuo wake. Tayari tumesoma thibitisho

la uumbaji, pamoja na uthibitisho wa ajabu ya janga lililotokea kabla ya Adamu na ushahidi wa kutosha wa gharika katika siku za Nuhu. Hili ni thibitisho linaloonekana kwa wale ambao wana macho ya kuona. Lakini ulimwengu mzima umefunga macho yake usione ukweli na “wamekaa gizani” kimakusudi (Yohana 12:46), Pia tumechambua thibitisho la unabii-ushahidi mkuu kwamba Mungu aliye hai, mtendaji, ndiye aliandika Biblia na kuuleta utimizaji wa unabii wake.

Wanaopuuzia kimakusudi pekee ndio wanaweza kukataa ushahidi wa uumbaji na unabii. Lakini, kwa huzuni, ulimwengu umejaa na watu kama hao! Wamekana yote.

Wingi wa ushahidi unalemea. Ni mkuu sana kiasi kwamba kozi ya Biblia haiwezi kuibeba yote. Lakini ushahidi mwingi umefanya ukweli kinzani. Kama vile ulimwengu unachapisha na kuuza Biblia, lakini hawajaamini Biblia, pia unavumbua, kuchapisha na kuuza ushahidi wa msukumo wa Biblia BILA KUAMINI USHAHIDI HUO!

Ulimwengu haujageuza ukweli peke yake lakini hata THIBITISHO pia -Wakifanya Ukweli UONEKANE kama uwongo na thibitisho la kweli LIONEKANE kama uwongo.

Ili nikusaidie uelewe ushahidi wa kushangaza, hakikisha Biblia yako iko mbele yako. Pia uwe na karatasi, na kalamu ya kawaida ama ya risasi ili uandike majibu ama maoni yako. Hamna maswali mengi katika somo hili kwa sababu tunakupatia thibitisho la Biblia lililotiwa msukumo na Mungu moja kwa moja kutoka REKODI ZA KIHISTORIA zenyewe.

Unapaswa uweke kwa muhtasari THIBITISHO JIPYA mwenyewe, katika neno lako. Hiyo ndiyo njia muhimu ya KUKUMBUKA thibitisho hayo!

Thibitisho haya yanaaibisha wakanaji.  
Thibitisho haya yanaonyesha mara moja  
kwamba rekodi ya kibiblia imetiwa  
msukumo na ni ukweli!

Je, uko tayari?

## SOMO LA 12

### Historia Inarekodi GHARIKA

Hapo awali, tumeonyesha ushahidi wa  
uumbaji na Sayansi. Sasa tunakuja kwa  
jaribio muhimu ya msukumo wa Biblia.

Biblia imebeba rekodi ya MATUKIO YA  
KIHISTORIA ambayo yamechukua muda wa  
miaka 4,000 ya uzoefu wa binadamu.  
KIHALALI MAELEZO MENGI ZAIDI YA ELFU,  
AMBAYO USHAHIDI WA KIHISTORIA  
UNABAKI, YANATURUHUSU KUTAMBUA  
IKIWA BIBLIA NI UKWELI-au ikiwa ni rekodi  
za itikadi ya kidhana na hekaya ambazo  
zilisanywa kwa njia isiyo sahihi karne  
nyingi baada matukio hayo na “kufanywa  
kuonekana” kama kazi ya Mungu, kama  
vile Dk. Moffatt na Goodspeed  
wanavyotamka.

Je, historia ya Biblia ni ukweli? Wacha  
TUTHIBITISHE KWA HAKIKA ikiwa  
tunaweza kutegemea Biblia kama  
UKWELI!

1. Je, Biblia inarekodi kwamba gharika  
kubwa ilitokea nyakati za Nuhu ambayo  
iliharibu karibu kila uhai wa dunia?  
Mwanzo 7:1, 6, 21, 22.

**MAONI:** Ikiwa mataifa yanatoka kwa  
familia moja, kama vile Biblia  
inavyofundisha, tunapaswa tutarajie  
mataifa yote yawe na mapokeo ya kale  
kuhusu gharika.

Katika somo lililopita tulithibitisha  
ushahidi wa KIJIOLOJIA wa gharika katika  
siku za Nuhu. Wakosoaji wanawezapinga  
wakati huo (kwa sababu wanakataa  
mpangilio wa Biblia), lakini wanajua  
REKODI zipo ambazo kila mtu anaweza  
kuziona. Ambazo hawawezi kukana! Na  
kama Nuhu na familia yake waliepuka

madhara ya gharika, hatuhitaji mambo  
mengi ikiwa tunatafuta uthibitisho  
miongoni mwa mataifa yote kwamba  
gharika ilitangulia kupatikana kwa  
mataifa ya leo.

Ni nini historia ya ushuhuda-ushuhuda  
ambao watu wamechimbua,  
wametafsiriri, wamechapisha na  
kusambaza kwa matumizi ya umma?

Hapa ndipo ukweli ambao kila mtu  
anaweza kujua: WAMAREKANI WAHINDI  
katika Kaskazini na Kusini mwa Marekani  
walihifadhi simulizi ya Gharika ambapo  
wachache waliepuka kwa njia ya  
kujifanyia watu wa dunia.

WENYEJI wa GRINILANDI walidumisha  
kwamba watu wote walipata kuzama na  
kwamba mwanamume na mwanamke  
walikuja kuwa wahenga wa ye yote  
anayeishi.

WAPOLINESI kutoka Pasifiki Kusini  
wanashindania kwamba gharika ililemea  
wote bali tu watu wanane.

Kimila ya KICHINA inaongea juu ya  
ustaarabu wake ya kwamba kimepatikana  
na mtu pamoja na vijana wake tatu na  
binti tatu, ambao waliepuka gharika  
kubwa.

Mapokeo ya WAAFRIKA NA WAMISRI,  
inahifadhi sababu hizo zinazofanana.

WAGIRIKI wanaangalia “Nuhu” kama  
kuijenga safina ili aepe maji mengi,  
baadaye akamtuma njiwa mara mbili  
kabla miguu yake haijagusa dunia tena.

WABABELI WA kale na ASHURU  
wametuhifadhia katika vibao vya udongo  
wa mfinyanzi neno baada ya jingine ya  
maelezo ya desturi miongoni mwao-  
mapokeo ambao ni kamili katika maelezo  
mengi!

Hebu fikiria kidogo-IKIWA Gharika  
haikutokea, je hawa watu wote  
wangehifadhi rekodi hizi za Gharika?  
Ukweli watu wote hawangedanganywa

kuamini Gharika ilitokea kama haikutokea! Kanisa la zamani la Mungu la Redio liliripoti kwamba, "Unaweza kupata ushuhuda usiojulikana ya mataifa ya kale katika Kamusi Elezo, makala "gharika kwa wingi" na kwa aina ya muhtasari katika kijitabu cha maelezo ya Biblia ya Halley. Ukitaka bonyeza <http://www.talkorigins.org/faqs/flood-myths.html>.

Hivyo basi, kwa Gharika ya Nuhu tunao ushahidi wa kweli NA ushuhuda wa watu wengi wa kale ambao walikumbuka matokeo ya janga hilo. Sababu ya kipekee ambayo inafanya watu wasiamini ni kwamba mwanadamu hana nia ya kuamini yanayosemwa na Mungu! Afadhali anaweza kuamini hekaya ya mageuzi kwamba vitu vimeendelea vile vilivyo kuanzia mwanzo wa wakati.

Baada ya kujua hakika hizi, wakanaji wengi wanasisitiza kwamba rekodi za kibiblia zilitoka kwa mapokeo ya kibabeli lakini sio ukweli. USHUHUDA HUU NI KINYUME! Karibu rekodi zote za Wababeli tunazo zinapatikana katika maktaba ya Arshurbanipali (mnamo 650 K. K), muda mrefu baada ya rekodi ya Musa kuhusu Gharika ya Nuhu. Maelezo timamu ni kwamba watu wengi walihifadhi matukio YAO. Kwa matukio haya yote rekodi ya kibiblia ndiyo haina utata na imejaa na urahisi uliosahihi.

Kwa hivyo Kitabu cha vitabu ni sahihi baada ya vyote MAANDIKO YANASIMAMA KUTHIBITIKA. KIMETIWA MSUKUMO. NI UKWELI KWA KILA NJIA!

## PASAKA: Je Inahusu Kifo cha Kristo Peke Yake?



*Je Wakristo wanapaswa kuadhimisha Pasaka?*

Na Bob Thiel

Vile wengi wanavyofahamu, wana wa Israeli waliambiwa haswa kuadhimisha Pasaka katika kitabu cha Agano la Kale cha Kutoka.

Kila familia ilichukua mwana-kondoo, ambaye hana hila (Kutoka 12:5), ya kuchinjwa (Kutoka 12:3-4). Mwana-kondoo alichinjwa siku ya kumi na nne jionin (Kutoka 12:6) na baadhi ya damu yake ilitiwa kwenye mlango wa kila nyumba ya familia (Kutoka 12:7). Waliochukua hatua vile Mungu alivyoamuru "walipitwa" na kifo, wakati ambapo Wamisri ambao hawakufanya hivyo hawakuachwa (Kutoka 12:28-30).

Kama vile wengi wanavyogundua, Yesu aliadhimisha Pasaka kila mwaka (Kutoka 13:10) kutoka wakati wa ujana wake (Luka 2:41-42) na kwa maisha yake yote (Luka 22:15).

Pasaka iliadhimishwa tarehe kumi na nne ya mwezi wa kwanza (Walawi 23:5; unaoitwa Abibu katika Kumbukumbu la Torati 16:1 au Nisani katika Esta 3:7). Inafanyika wakati wa Majira ya kuchipua ya mwaka.

Ijapokuwa Yesu alibadilisha utendaji mwingi uliohusiana na Pasaka (Luka 22:19-22; Yohana 13:1-17), Mwakozi wetu pia aliwaambia wanafunzi wake waadhimishe Pasaka (Luka 22:7-13). Pia Agano Jipya ni wazi, kwamba kwa sababu ya kifo cha Yesu, kuchinja kondoo na kutia damu kwenye miimo ya mlango

(Kutoka 12:6-7) haihitajiki tena (Waebrania 7:12-13,26-27;9:11-28).

Mtume Paulo alifundisha kwamba Wakristo wanapaswa kuadhimisha Pasaka kulingana na maagizo ya Yesu (1 Wakorintho 5:7-8; 11:23-26).

Biblia inafundisha kwamba Yesu "amejulikana kweli tangu zamani, kabla haijawekwa msingi wa dunia (1 Petro 1:20) kuwa "Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia (Ufunuo 13:8). Kwa hivyo, mpango wa Mungu kupitia kwa Siku Zilizotakatifu na Siku Kuu zake, pamoja na Yesu kuwa "Mwana-Kondoo wa Pasaka," ulijulikana Kabla wanadamu hawajawekwa duniani. Hii ndiyo sababu vifaa vya mbingu viliwekwa ili visaidie kuhesabu siku hizo!

Ni vizuri kwamba makanisa yanagundua kwamba Biblia inafundisha kwamba Yesu alitimiza vitu vingine vilivyohusu Pasaka wakati aliuawa.

Tunapata uendeshaji wa dhabihu hii mkuu hata imejadiliwa katika Bustani wa Edeni. Baada ya Yesu kutabiriwa (Mwanzo 3:15), Mungu alimua mnyama (labda ni kondoo ama mbuzi), ili afunike uchi (unaonyesha aina ya dhambi katika tukio hili) wa Adamu na Hawa na ngozi ya mnyama huyo (Mwanzo 3:21). Tunaona pia kanuni ya dhabihu ikiendeshwa wakati Abeli alitoa dhabihu kutoka kwa mifugo yake (Mwanzo 4:2-4).

Pasaka iliojulikana katika siku za Musa ilionyesha ukombozi wa wana Israeli kutoka Misri (Kutoka 12:1-38). Musa alirekodi maagizo kuhusu Pasaka na pia kalenda yake (Mwanzo 1:14; 2:1; Kutoka 12:1) na Siku Kuu zake (Walawi 23). Pasaka kimsingi ikawa ya kwanza kwa matukio haya ambayo yanaonyesha wana wa Mungu Mpango wake mkuu wa wokovu.

Katika Agano la Kale, Pasaka inaonyesha ukombozi kutoka kwa Misri na kuingilia kati kwa Mungu. Lakini, kiunabii, ilikuwa

inaonyesha wakati Yesu angekuja kuwa Mwana-kondoo wa Pasaka (1 Wakorintho 5:7). Mwana-Kondoo wa Mungu aliyekuwa kuondoa dhambi za ulimwengu (Yohana 1:29; 3:16-17).

Wakati Yesu alifanya Pasaka ya mwisho akiwa mwanadamu, aliendelea kuadhimisha Pasaka jioni na kuwaambia wanafunzi wake kufanya hivyo (Luka 22:14-19; Yohana 13:2,12-15) na katika tarehe 14 ya Nisani/Abibu (Luka 22:14;23:52-54).

Yesu, hata hivyo, alibadilisha utendaji mwingi uliohusiana na maadhimisho yake. Yesu alitengeneza mkate na divai kuwa sehemu muhimu ya Pasaka (Mathayo 26:18,26-30) na akaongeza utendaji wa kutawadha mguu (Yohana 13:12-17).

Yesu hakufundisha kwa njia yo yote kwamba Pasaka haifanywa kila mwaka, wala hakubadilisha wakati wa siku ya kuadhimisha kuwa Jumapili asubuhi kama vile wanavyofuata desturi ya Wagiriki-Rumi wanavyofanya. Hata wasomi wa Griki na Othodoksi (Jimbo kuu la Othodoksi Ugiriki la Marekani) wanakubali kwamba Wakristo wa karne ya 1 na 2 waliadhimisha Pasaka usiku kama vile sisi tulio katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) tunafanya katika karne ya 21 (Calivas, Alkiviadis c. The Origins of Pascha and Great Week-Part 1,1992).

Pengine inafaa iongezwe kwamba Kanisa la Rumi (na waprotetani waliotoka kwake) wanafundisha kwamba wanaadhimisha Pasaka, lakini wamempa jina tofauti sana katika lugha ya Kiingereza na pia hawaadimishi kama vile Yesu alivyofanya (Catechism of the Catholic Church, 1995).

### **Pasaka Ilikuwa Tarehe 14 siyo 15**

Wengi wamechangikiwa kuhusu tarehe ya Pasaka ya kibiblia. Biblia inafundisha kwamba inafaa iadhimishwe tarehe 14 ya



mwezi wa kwanza wa kalenda ya Mungu (Walawi 23:5).

Katika mstari wa 6 wa Kutoka 12, inaonyesha kwamba mwana-kondoo angechinjwa “jua lituapo” (GWT and Jewish Publications Society translations). Mstari wa nane inasema kwamba wangekula nyama yake usiku huo, ingeokwa na kuliwa usiku huo. Na kama mtu ambaye amechinja kondoo, mtu anaweza kuchinja, kuoka, na kumla kondoo 'wa mwaka mmoja' (Kutoka 12:5) kati ya jioni na usiku wa manane-ambao Waisraeli walifanya kwenye Pasaka iliyorekodiwa katika Kutoka 12. Kiufundi, walikuwa nayo hadi asubuhi ili wapate kuwala kulingana na (Kutoka 12:10). Basi Biblia ni wazi kwamba Pasaka ya kimalaika ilifanyika “usiku huo” (Kutoka 12:12), usiku huo huo wa tarehe 14.

Biblia inafundisha kwamba Yesu angechinjwa mara moja (1 Petro 3:18; Waebrania 9:28; 10:10-14). Katika Agano Jipya, ni wazi kwamba Yesu aliadhimisha Pasaka yake ya mwisho (Luka 22:14-16), na akauawa. Biblia inaonyesha kwamba Yesu alitolewa mtini kabla ya tarehe 15. Kwa nini? Kwa sababu tarehe 15 ilikuwa “siku kubwa” (Yohana 19:28-31), hasa ilikuwa siku ya kwanza ya mkate usiotiwa chachu (Walawi 23:6). Kwa hivyo, Yesu aliadhimisha na kutimiza Pasaka tarehe 14.

Historia ya awali ya kanisa pia inarekodi kwamba Pasaka iliadhimishwa tarehe 14 ya mwezi wa Nisani na Wayahudi waaminifu na viongozi wa Wakristo wa mataifa katika karne ya kwanza, ya pili na ya tatu na iliadhimishwa jioni.

Viongozi wengi wanaokiri Kristo wanadai kuadhimisha Pasaka hiyo, ijapokuwa wamebadilisha jina, tarehe, wakati, na ishara, na maana-siku inayojulikana kama “Easter” katika Kiingereza ilipaswa kuwa Pasaka kulingana na makanisa ya Wagiriki-Rumi wa awali.

Biblia inatufundisha vyema kwamba Yesu Kristo ndiye alikuwa Mwana-kondoo wa Pasaka kwetu sisi na kwamba inafaa tuadhimishe Siku kuu hiyo na mkate usiotiwa chachu:

7 Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani Kristo; 8 basi na tuifanye karamu, si kwa chachu ya kale, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, bali kwa yasiyochachika, ndio weupe wa moyo na kweli. (1 Wakorintho 5:7-8)

Kumbuka kwamba karamu hii inafaa kuadhimishwa na mkate usiotiwa chachu wa weupe wa moyo na ukweli. Mtume Paulo aligundua kwamba Yesu alitumika mbadala wa mwana kondoo wa Pasaka ambaye Wayahudi walitumia. Alifundisha kwamba Wakristo wanapaswa kuendelea mbele na kuadhimisha Pasaka.

Lakini kimsingi ni jinsi gani Wakristo wangepaswa Pasaka?

Mtume Paulo anaeleza:

23 Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule alitolewa alitwaa mkate, 24 naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. 25 Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. 26 Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. 27 Basi kila aulaye makte huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia

hatia ya mwili na damu ya Bwana. 28 Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. 29 Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. (1 Wakorintho 11:23-29).

Kwa hivyo, Mtume Paulo alifundisha kwamba Wakristo wangeadhimisha Pasaka kwa namna ile Yesu aliadhimisha Pasaka yake ya mwisho na Mkate kwa divai. Na hiyo ilikuwa usiku kama kumbukumbu au kumbusho-kumbusho inafanywa baada ya mwaka, silo tukio la kila wiki.

*Katekismo ya kanisa la Katoliki* imeandika vizuri kwamba “Yesu alichagua siku ya Pasaka... akachukua mkate, na ... akagawa” na akatoa uliwe.

Imeandika katika Biblia kwamba Yesu alipasua mkate usiochachwa na kuwapa wanafunzi wake ili wale. Yesu pia aliwapa wanafunzi wake divai ili wanywe kidogo. Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) twaomba, tunapasua na kugawa mkate usiochachwa, na kugawa divai kwa wanafunzi waaminifu ili waumege na kunywa kikombe hicho. Na bado kanisa la Rumi (kama vile makanisa mengine) hawavunji mkate usiochachwa (linatumia mkate ulio na chachu) na hata wakati mengine hawagawi divai kwa waumini wao ili wanywe (ugawaji wa divai inachukuliwa kwamba si lazima na kanisa la Rumi, na mara nyingi haufanywi na makanisa ya Waprotestani.)

**Nini inahusu 'Kila Mkifanya... Mwaitangaza'?**

Ni mara ngapi Pasaka inafaa ifanywe?

Yesu alisema, “Kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.”

Kumbuka kwamba ni mauti ya Yesu ndiyo Pasaka inaadhimisha.

Kifo cha Kristo kinatupatanisha na Mungu (Warumi 5:10) na Yesu alitoa uhai wake kwa wokovu wetu (Yohana 3:16-17; Waebrania 5:5-11). Kifo chake kinatufundisha kwamba miili ya Wakristo haifai kutawalwa na dhambi (Warumi 6:3-12). Pasaka ya Wakristo ni maadhimisho ya kifo cha Yesu kila mwaka.

Yesu HAKUSEMA tufanye siku kuu KILA MARA UNAVYOTAKA, bora tu ufanyapo, unatangaza kifo chake. Neno la Ugiriki ya kila mara katika 1 Wakorintho 11:26, hosakis, limetumika mahali pengine katika Agano Jipya. Halimaanishi kila mara mnapotaka ILA istilahi ya Ugiriki ya “mfanyapo”, *thelo* au *ethelo* pia ni ya wakati uliopo (ambayo inapatikana katika Ufunuo 11:6; sehemu katika Biblia ambayo istilahi hii imetumika). Hata hivyo, kwa vile neno hili silo la wakati uliopo katika 1 Wakorintho 11:26, Paulo hakutuambia tuadhimisha Pasaka ya Bwana kila wakati tukitamani, lakini wakati tunapoadhimisha katika siku hiyo ya Pasaka, siyo tu sherehe, inaonyesha kifo cha Yesu.

Zaidi ya hayo, Paulo aliandika haya:

27 Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. 28 Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. 29 Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. (1 Wakorintho 11:27-29)

Paulo anafundisha kwamba ili umege mkate huu na kukunywa divai hii, mtu lazima ajichunguze. Kuondoa chachu ambako kunafuata Pasaka kunatusaidia kuzingatia makosa yetu na dhambi zetu na hivyo linatimiza agizo la Paulo ili tujichunguze. Kama vile kuondoa chachu inahitaji juhudi nyingi, hii pia inaunga

mkono dhana ya kujichunguza kila mwaka (watu hawakuwa wakiondoa chachu kila siku ama kila wiki.)

Agano Jipya linafundisha kwamba Paulo na Yesu walifundisha maadhimisho ya Pasaka katika njia ya Ukristo.

### **Kutawadha Mguu**

Kutawadha mguu inatusaidia kuonyesha unyenyekevu na kwamba hata wanafunzi wa Kristo bado walikuwa na sehemu ambazo zilikuwa zinahitaji kusafishwa (Yohana 13:10).

Yesu alifundisha kwamba Wanafunzi wake wanapaswa kufanya hivyo:

13 Ninyi mwaniita Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. 14 Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu ninyi kwa ninyi. 15 Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo. 16 Amin, amin, nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. 17 Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda. (Yohana13:13-17)

Wachahe ambao wanakiri Ukristo wanatawadha miguu kama vile Yesu alisema ifanywe. Lakini sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) tunafuata maagizo ya Yesu kwa kufanya hivi kila mwaka.

### **Vyanzo Nje ya Maandiko**

Siyo katika Biblia tu ambapo tunaona kwamba Pasaka iliadhimishwa na Wakristo kila mwaka. Historia inarekodi kwamba waaminifu waliadhimisha Pasaka kila mwaka kwenye tarehe. 14 kuanzia wakati wa mitume wa awali na kote katika vizazi vyote.

Kuna maelezo mengine yanayovutia katika nakala mbaya inayojulikana kama *Maisha ya Polikapu*. Kinachovutia ni kwamba inapendekeza kwamba maadhimisho ya Pasaka katika Asia Ndogo hayakuja kwanza Smirna kutoka kwa Mtume Yohana, lakini hata hapo awali hayakutoka kwa Mtume Paulo.

Maisha ya Polikapu yanapendekeza kwamba Pasaka ya Agano Jipya na mkate usiotiwa chachu na divai ingeadhimishwa kwa msimu wa mkate usiochachwa. Inaonyesha kwamba wazushi waliadhimisha siku hiyo kwa njia tofauti. Na andiko hilo pia inapendekeza dhana kwamba mkate usiochachwa NA divai ilitumika, na ilitumika KILA MWAKA.

Historia inarekodi kwamba Mitume ambao wameorodheshwa kwa Biblia (ikiwa ni pamoja na Filipo na Yohana) na pia Waaskofu/Wachungaji Polikapu, Thrasesi, Sagarisi, Papirasi, Polikrati, Apoloniri na wengine waliadhimisha Pasaka kila mwaka katika tarehe 14. Warumi, Othodoksi ya Mashariki, na Anglikana Wakatoliki wote wanaamini kwamba hao viongozi walikuwa watakatifu, na bado madhehebu hayo wanafuata vielelezo vya hao watakatifu.

Mwanahistoria Usebia aliripoti kwamba Askofu/Mchungaji Apolonira ya Hieropolisi katika Frigia ya Asia Ndogo aliandika katika karne ya pili ikiisha kwamba Wakristo wangedhimisha Pasaka tarehe 14.

Siku ya kumi na nne, Pasaka ya kweli ya Bwana; sadaka kuu, Mwana wa Mungu badala ya mwana-kondoo, alishikwa... na kuzikwa katika siku ya Pasaka, na jiwe likawekwa kwenye kaburi lake.

Yesu alikula na kuadhimisha Pasaka tarehe 14, akauawa tarehe 14, na akazikwa tarehe 14. Hii haikuwa tarehe 15, na katika mwaka wa kifo chake, haikuwa siku ya Jumapili. Yesu

angechukua Pasaka baada ya jua kutua na angeuawa mchana na kuzikwa kabla ya machweo pia (ambayo inianza siku mpya).

Katika karne ya pili ikiisha, Askofu/ Mchungaji Polikrati wa Efeso alituma barua kwa Askofu wa Kirumi Victor wakati Victor alijaribu kulazimisha maadhimisho ya Pasaka siku ya Jumapili badala ya tarehe 14.

Katika barua yake, Polikrati:

- 1) Alisema anayafuata mafundisho yaliyotoka kwa Mtume Yohana.
- 2) Alisema kwamba yeye anabaki kuwa mwaminifu kwa Injili.
- 3) Alitegemea kwa msimamo kwamba mafundisho kutoka kwa Biblia yalikuwa vyema kuliko mapokeo ya Kirumi yaliyokubalika.
- 4) Alisema anabaki kuwa mwaminifu kwa mafundisho aliyopokea kutoka kwa viongozi wa kanisa la awali.
- 5) Alionyesha kwamba alikuwa msemaji wa waumini waliokuwa Asia Ndogo.
- 6) Alisema kwamba yeye na waliaomtangulia waliadhimisha nyakati za siku kuu za mkate usiotiwa chachu.
- 7) Alikataa kukubali mamlaka ya mapokeo yasiyo ya kibiblia ya Warumi dhidi ya Biblia.
- 8) Alikataa kukubali mamlaka ya Askofu wa Rumi-alichagua kuwa tofauti (Ufunuo 18:4).
- 9) Alisema kwamba maisha yake ungetawalwa na Yesu na maoni ya watu.

Je, unaweza kuufuata mfano wa Yesu na Mtume Polikrati vile walivyofanya?

Kwa sababu Wakristo waliadhimisha Pasaka tarehe 14, wao na wengine walipewa jina Kuotadesimani (Quartodecimans) (Lugha ya Latini inayomaanisha kumi na nne) na wahistoria wengi.

Wakristo wa awali waligundua kwamba Pasaka ilikuwa inaonyesha Mpango wa Mungu wa wokovu. Kumbuka kwamba mnamo 180 B.K., Askofu/Mchungaji Melito wa Sarde aliandika:

Alafu ikaja siri ya Pasaka, hata vile imesimama imara ilivyoandikwa katika sheria... Watu basi wakawa mfano wa kanisa na sheria ikawa mchoro wa kimfano. Lakini injili ikawa maelezo ya sheria na utimizaji wake, wakati Kanisa likawa nyumba ya akiba ya ukweli... Hii ni pasaka ya wokovu wetu. Huyu ndiye alivumilia vitu vingi miongoni wa watu... Huyu ndiye alikuwa mwanadamu katika bikra, aliyesulubiwa mtini, ambaye alizikwa ardhini, aliyefufuka kutoka kwa wafu, na aliyefufua binadamu kutoka kwa kaburi lake chini hadi akaonekana juu karibu mbingu. Huyu ndiye mwana-kondoo aliyechinjwa.

Pasaka iliadhimishwa kila mwaka tarehe 14 ya Nisani na waaminifu na wengine katika karne nyingi. Wasomi Wakatoliki wanarekodi kuwa ilifanyika tarehe 4, 5, 6-8 na karne nyingi baadaye. Waandishi tofauti wa makanisa ya Mungu wamefuata maadhimisho yake kutoka nyakati za mitume hadi nyakati hizi.

Wasomi kutoka Wagiriki-Rumi wamegundua kipengele cha Pasaka, kama kutawadha mguu, iliadhimishwa na wale waliojulikana kama Wakristo waaminifu wa awali.

Pasaka ndiyo Siku kuu ya kwanza ya kila mwaka iliyoorodheshwa katika sura ya 23 ya Mambo ya Walawi. Pasaka inasaidia

kuonyesha wokovu na neema ya Wakristo. Inafaa ijulikane kwamba Wakristo wa awali waliita Pasaka lakini siyo "Mesa ya Bwana." Wakati wengine wanaweza "kuweka kiroho" umuhimu wa maadhimisho ya Pasaka, viongozi wanaojulikana kama watakatifu na Wagiriki-Rumi na Kanisa la Mungu waliadhimisha Pasaka kama ilivyoagizwa.

Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) bado tufanya hivi hadi leo. Tunaadhimisha Pasaka kwa kuzingatia vitendo vya historia za kibiblia ya kutawadha miguu.

### **Mpango Kutoka Mwanzo**

Pasaka inaonyesha kwamba Mungu alikuwa na mpango kabla ya kuweka msingi wa ulimwengu (1 Petro 1:20) kumtuma Yesu atufie dhambi zetu, ya kwamba Mungu anatupenda (Yohana 3:16), ya kwamba Mungu anaweza kutuokoa, na kwamba Mwana wake aliteswa na kutufia. Pasaka inaonyesha kwamba Wakristo wamewekwa huru kutoka kwa dhambi kwa kifo chake na hivyo hawafai kubaki katika dhambi (Warumi 6:15).

Lakini kuikubali tu dhabihu ya Yesu peke yake siyo mpango wote wa Mungu wa wokovu.

Watu wengi wanaadhimisha mwanzo wa siku kuu za Mungu ya wokovu kwa kugundua kwa kiasi fulani Pasaka na/ama Pentekoste, laini hawaendelei "kugundua kina cha utajiri" (Warumi 11:33) wa neema ya Mungu (2 Petro 3:18) inaoyonyeshwa na siku kuu zingine za Biblia.

Wakristo wanapaswa kuadhimisha Pasaka. Na kuiadhimisha kwa njia ya kibiblia.

Kristo ndiye mwanzilishi wa wokovu wetu (Waebrania 5:9), na pia yeye ndiye

anayetimiza wokovu wetu (Waebrania 12:2;1 Petro 1:1-9). Wafuasi wake wa ukweli wanaadhimisha SikuTakatifu ya majira ya machipuko na majira inayopatikana kati ya majira ya kiangazi na baridi. Kwa maelezo mengi, tafadhali soma kijitabu chetu, "Je unapaswa kuadhimisha Siku kuu za Mungu ama sherehe za kipepo? Kinapatikana kwenye tovuti ya [www.ccog.org](http://www.ccog.org)

**Kuitekeleza Mathayo 24:14  
Pamoja na Mathayo 28:19-20**

**Kanisa la Mungu Linaloendelea(CCOG)**

**[www.ccog.org](http://www.ccog.org)**

**Taarifa za Unabii wa Biblia zan kila siku**

**[www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com)**



**CCOG.ASIA:Hii ni Tovuti ilengayo wasomaji kutoka Asia.**

**Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.**

**CCOG.EU:Hii ni Tovuti kwa wale wa Ulaya.Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.**

**CCOG.IN:Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Kihindi.**

**CCOG.NZ:Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya New Zealand.**

**CCOGCANADA.CA:Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya Canada.**

**CDLIDD.ES:Hii ni Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) katika lugha ya Kihispania.**

**PNIND.PH:Hii ni Tovuti kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.**



**Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia:**

**[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](http://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)**

**Chaneli ya Kanisa la Mungu Linaloendelea(CCOG):**

**[www.youtube.com/continuingcog](http://www.youtube.com/continuingcog)**

**Kanisa la Mungu Linaloendelea(CCOG)**

**pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielektroniki,vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika kutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-20.**

